

**CHANGAMOTO ZA KUTAFSIRI MATINI ZA KISHERIA: TATHMINI YA
KATIBA YA KENYA (2010)**

**Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili
wa sanaa (Kiswahili) katika Chuo Kikuu Cha Nairobi.**

NOVEMBA 2014

Ikirari

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijapata kutolewa na mtu mwingine kwa mahitaji ya shahada katika chuo kingine chochote

NJENGA GRACE WAITHIRA (mtahiniwa) Tarehe

Tasnifu hii imeandikwa chini ya usimamizi wetu,

DKT. ZAJA OMBOGA Tarehe

DKT. NYACHAE MICHIRA Tarehe

Tabaruku

Tasnifu hii nawatabarukia wazazi wangu wapendwa, Bw Charles Njenga na Bi Rose Wanjiru. Wao ndio walinitia azma yangu ya kusoma na kuhakikisha kuwa nimefanikiwa kuitimiza azma hiyo.

Mume wangu mpendwa Martin Kariuki kwa kuniruhusu kurudi darasani licha ya kuwa na majukumu mengine kama mke. Wanangu wapendwa Njenga, Mihang'o na Njoroge kwa kuwanyima wakati wao waliouhitaji kutoka kwa mama. Kitoto Wangari kwa kunivumilia nifanye kazi hii.

Shukrani

Kwanza ni kwa Mwenyezi Mungu kwa umbali niliotoka na mahali amenifikisha kwa kweli nimetambua kwamba Yeye ni **EBENEZER**.

Pili nawashukuru wasimamizi wangu Dkt. Zaja Omboga na Dkt. Nyachae Michira ambao waliningoza ipasavyo. Bila mwongozo wao singeweza kuwasilisha mawazo yangu kuhusu suala hili kwa ukamilifu.

Tatu nawashukuru waalimu walioniandaa kuweza kuimudu kazi ya kitaaluma kiasi hiki. Waalimu hawa ni Dkt. Iribe, Prof. Habwe, Dkt. Mbuthia, Dkt. Mweri, Dkt. Amri Swale, Prof. Kineene wa Mutiso, Bw. Mungania na Prof. Mwenda Mbatia.

Ningetaka pia kuwashukuru wenzangu tuliokuwa nao baharini. Hawa ni Scholastica Waweru, Ruth Binyanya, Jael Akinyi, Vincent Oiro, Magdalene Mulwa, Sister Teresiah Waweru, Regina Gitau, Julius Mwangi, Beatrice Kisakwa, Margaret Karanja, Furaha Mbetsa, Mariamu Ngome, Duncan Munga, Samwuel Tsuma, Dorice Kachipera, Jane Obara, Margaret Muthoni na Nahason Akunga. Tulitiana moyo, tukashauriana na tukasaidiana mambo yalipokuwa magumu.

Shukrani zingine ziwaendee wazazi wangu Charles na Rose kwa malezi mema mlionipa Mungu awabariki sana.

Shukrani za dhati ni kwa mume wangu Martin, hata kama hukusema mengi ulisimama nami hadi nikakamilisha kuandika tasnifu hii.

Mwanangu Njenga nilikuachia kazi ya kuwalea nduguzo Mihang'o na Njoroge na ukanipa fursa ya kuingia darasani. Mungu akujalie ufikie malengo yako maishani. Wanangu Mihang'o na Njoroge kwa kuvumilia, hata ingawa hamkuelewa yaliyoendelea mlijua naenda shuleni na mkanipa nafasi ya kufanya 'homework'. Kitoto Wangari kwa kunipa 'moral support' kama walivyozoea kuniambia wenzangu ukiwa ungali tumboni. Mwisho ningependa kumshukuru mpwa wangu Jane Wambui, kwa kusaidia katika malezi ya wanangu ili niweze kurudi darasani na vilevile kuipiga chapa tasnifu hii. Ilikuwa kazi yenye uchovu mwingi na uliifanya bila kulalamika. Mungu akubariki sana. Mwingine aliyenisaidia kupiga chapa kazi yangu bila kuchoka ni Nellie, pokea shukrani zangu. Shukrani ni kwa wengine wote waliochangia kufaulu kwangu katika kazi hii kwa njia moja au nyingine. Singeweza kutaja majina yenu yote, pokeeni baraka zake Mwenyezi Mungu.

Yaliyomo

Ikirari.....	ii
Tabaruku	iii
Shukrani	iv
Yaliyomo.....	vi
Ikisiri	ix
Vifupisho ya maneno	x
SURA YA KWANZA	1
1.1 Utangulizi wa somo la utafiti.....	1
1.2 Tatizo la utafiti.....	3
1.3 Malengo ya utafiti	5
1.4 Nadharia Tete.....	5
1.5 Sababu za kuchagua mada hii	5
1.6 Upeo na Mipaka.....	6
1.8 Yalioandikwa Kuhusu Mada hii.	9
1.9 Njia za utafiti.....	13
SURA YA PILI.....	15
Ujumla na upekee wa Tafsiri za kisheria.....	15
2.1 Dhana ya Tafsiri.....	15
2.2 Dhima ya Tafsiri	18

2.3 Nadharia za Tafsiri.....	19
2.4 Uainishaji wa Matini za Kisheria.....	20
2.5 Sifa za Kijumla za Matini za Kisheria	23
2.6 Sifa za Katiba kama Matini ya Kisheria	30
2.7 Changamoto za Kutafsiri Matini za Kisheria.....	33
2.8 Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto za Kutafsiri Matini za Kisheria	35
2.9 Hitimisho.....	36
Tathmini ya sura ya kumi na moja ya katiba ya Kenya (2010)	37
3.0 Utangulizi.....	37
3.1 Ufafanuzi wa sura ya kumi na moja ya katiba.....	37
3.2 Uwasilishaji wa Data kama ilivyo katika sura ya kumi na moja ya katiba.....	38
3.3 Hitimisho.....	47
SURA YA NNE.....	49
Changamoto za kutafsiri matini za kisheria.....	49
4.0 Utangulizi.....	49
4.1 Ukosefu wa Ulinganifu wa Kiistilahi	49
4.2 Matatizo ya kileksia	50
4.3 Matatizo ya Kisintaksia.....	55
4.4 Matatizo ya Kisemantiki	57
4.5 Mikakati ya Kukabiliana na Ukosefu wa Ulinganifu wa Kiistilahi	60
4.6 Hitimisho.....	61

SURA YA TANO	63
Hitimisho, mafanikio, matatizo na mapendekezo	63
5.0 Utangulizi.....	63
5.1 Muhtasari	63
5.2 Hitimisho.....	64
5.3 Mafanikio na Matatizo	66
5.4 Mapendekezo	66
Marejeleo	68

Ikisiri

Kutafsiri matini za kisheria huwa na changamoto nyingi. Changamoto hizi husababishwa na sifa za kiisimu kama vile leksia, sintaksia, semantiki na pragmatiki. Kunayo mambo mengine ambayo si ya kiisimu kama vile tofauti za tamaduni za jamii husika na tofauti za kihistoria ambazo pia huzua changamoto katika kutafsiri matini za kisheria. Kazi hii imeshughulikia changamoto za kiisimu za kutafsiri sheria. Hii imefanywa kwa kutathmini sura ya kumi na moja ya katiba ya Kenya na kutoa mifano mahsusi ya changamoto hizi kama zinavyojitokeza katika sura hii. Dhana za tafsiri zimeelezewa kwa ujumla. Sifa za kijumla za matini za kisheria zimefafanuliwa kwa uwazi na maelezo yakatolewa ya jinsi sifa hizi zinavyoathiri tafsiri za matini za kisheria kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Vilevile mikakati ya kukabiliana na changamoto hizi imeelezewa kwa kina.

Vifupisho ya maneno

L.C ----- Lugha chanzi

L.L-----Lugha lengwa

M.C-----Matini chanzi

M .L-----Matini lengwa

SURA YA KWANZA

1.1 Utangulizi wa somo la utafiti

Tafsiri ni uwasilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha moja hadi nyingine. Catford (1965:20) anasema kuwa kutafsiri ni kuchukua mawazo yaliyo katika maandishi katika lugha moja (lugha chanzi) na kuyaweka badala yake mawazo yanayolingana katika lugha ya pili (lugha lengwa). Kwa mujibu wa Larson (1984), tafsiri huhusiana na kuhamisha maana ya makala asilia hadi katika makala tafsiri kwa kuzingatia muundo wa semantiki. Tafsiri ina jukumu la kuhamisha maana inayopatikana katika matini chanzi na kuiwasilisha katika lugha pokezi.

Licha ya kwamba tafsiri ni uwasilishaji wa maana, uwasilishaji huu hujitokeza kwa njia mbalimbali katika nyanja tofauti. Hii ina maana kuwa uwasilishaji wa maana katika tafsiri za kazi za kubuniwa kama vile fasihi huwa tofauti na jinsi maana huwasilishwa katika kazi halisi kama vile matini za kisheria, teknolojia na matibabu. Hii ni kwa sababu aina hizi za tafsiri huwa katika kategoria tofauti za tafsiri. Fasihi ni tafsiri ya kawaida ilhali sheria ni tafsiri ya kiufundi. Kila kategoria huhusisha matumizi tofauti ya lugha na huwa na upekee wake. Ili kuweza kufanikisha mchakato wa tafsiri, matini za tafsiri huainishwa. Newmark (1988:13) anapendekeza matini ziainishwe kwa njia tatu kuu. Njia hizi ni; matini elezi, matini arifu na matini amili. Matini elezi ni aina za matini ambazo huegemea zaidi kwa mwandishi. Mwandishi hutumia lugha kuelezea hisia zake bila kujali jinsi maelezo hayo yatakavyopokelewa na wasomaji. Mifano ya matini elezi ni pamoja na nyaraka za kisiasa, nyaraka za kisheria na nyaraka za kisayansi.

Matini arifu nazo ni matini zinazohusu mada yoyote ile ya maarifa kwa mfano biashara, uchumi n.k. Kwa kawaida matini hizi huwa katika maumbo sanifu mathalani vitabu, ripoti za kiufundi, makala katika magazeti n.k. Matini amili nazo ni zile ambazo huegemea upande wa wasomaji. Matini hizi hulenga kuibua hisia za wasomaji. Matini hizi ni kama vile matangazo, na fasihi pendwa.

Katika utafiti huu tutajikita katika tafsiri za matini elezi, hususan matini za kisheria. Uandishi wa kisheria huwekwa katika kategoria mbili kuu : uchanganuzi wa kisheria na usawidi wa kisheria. Utafiti wetu utajikita katika usawidi wa kisheria. Usawidi wa kisheria ni kule kuandika kwa mara ya kwanza makala ya kisheria kabla ya kufanya marekebisho ya mwisho. Usawidi hali kadhalika unahusu kuandika kwa njia zinazoakisi masharti, matarajio, maelezo, maelekezi na utoshelevu wa kisheria kwa jumla. Usawidi huu huhusu uandishi wa aina nyingi za matini za kisheria kama vile uandishi wa kandarasi, mikataba , katiba n.k. Matini hizi hutofautiana katika mitindo yake ya uandishi. Nchini Kenya lugha inayotumika kusawidi matini hizi ni lugha ya Kiingereza. Matini hizi hutafsiriwa baadaye kwa lugha zingine kutegemea matakwa ya wanazozitumia. Kulingana na katiba ya Kenya (2010) Kifungu cha 7, ibara ya 1&2, lugha ya Kiswahili imepewa hadhi ya kuwa lugha ya taifa na vilevile lugha rasmi nchini. Hii ina maana kuwa kila stakabadhi itakayotolewa kwa lugha ya Kiingereza lazima itafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili ili kukidhi matakwa ya kikatiba.

Kutafsiri matini za kisheria kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili huwa na changamoto nyingi. Utafiti huu unanua kuonyesha changamoto za kiisimu za kutafsiri matini za kisheria. Changamoto hizi huletwa na sifa za kiisimu za matini za kisheria na vilevile sifa zingine ambazo si za kiisimu. Lugha ya sheria ni lugha inayohusu sheria na lugha inayotumika katika mawasiliano ya kisheria.

Ni sajili ya lugha ambayo hutumika katika miktadha ya kisheria. Lugha ya sheria hutambulishwa na hali ya matumizi ya lugha sanifu, lugha tendaji na lugha ya kiufundi. Usanifu wa lugha hutokana na sababu kuwa, sheria huwa na jukumu la kimsingi katika jamii la kuongoza tabia za watu na kudhibiti mahusiano yao. Lugha inayotumika katika sheria ili kufikia lengo hili huwa ni elekezi, fafanuzi, na ya kuamuru. Ni lugha ambayo huhusishwa na kutunga kwa kanuni na kuzionyesha kanuni hizo.

Tafsiri za matini za kisheria pia huathiriwa na mambo mengine ambayo si ya kiisimu. Sheria na lugha ya kisheria hufungamana na historia, ukuaji na tamaduni za mfumo wa sheria. Mifumo ya kisheria huwa na upekee wa kijamii. Kila jamii huwa na mfumo tofauti wa kitamaduni, kijamii na kiisimu. Dhana za kisheria, mila za kisheria na utekelezaji wa sheria hutofautiana kutegemea jamii husika. Sheria ya taifa fulani huwa ni mfumo huru wa kisheria ulio na istilahi zake, dhana zake na kanuni zake za uainishaji. Sheria hizi hutofautiana kutoka taifa moja hadi nyingine. Jambo hili huzua changamoto wakati wa kutafsiri kutoka mfumo mmoja hadi mwingine. Hii ni kwa sababu istilahi nyingi katika lugha moja haziambatani na istilahi katika lugha nyingine.

Ili tuweze kuonyesha changamoto hizi za kutafsiri matini za kisheria tutatumia katiba ya Kenya (2010). Tutatathmini sura ya kumi na moja ya katiba ya 2010 na tafsiri yake ya lugha ya Kiswahili.

1.2 Tatizo la utafiti

Tatizo letu la utafiti ni kuchunguza changamoto za kutafsiri matini za kisheria kama zinavyojitokeza katika sura ya kumi na moja ya katiba tukitumia misingi ya kiisimu. Tunanua kuonyesha jinsi sifa za kiisimu za lugha ya kisheria huleta

matatizo wakati wa kutafsiri sheria. Katiba ni muhimu sana katika nchi na kwa hivyo tafsiri mwafaka inahitajika. Kunayo mambo mapya yaliyoongezewa katika katiba hii ya 2010. Mojawapo ni ugatuzi. Sura ya kumi na moja ya katiba inahusu ugatuzi. Kwa vile ugatuzi na mifumo ya ugatuzi ni mambo mapya yanayotanguliza dhana mpya, kuna uwezekano wa matatizo mbalimbali kutokea katika tafsiri. Matatizo haya yanaweza kutokana na ukosefu wa ulinganifu wa kiistilahi. Ukosefu huu unaweza kuleta changamoto katika uwasilishaji wa maana. Ugatuzi ni ile hali ya kugawa mamlaka kutoka serikali kuu hadi kwa serikali za kiwango cha chini. Ugatuzi huwa na michakato mingi kama inavyoelezewa katika sura ya kumi na moja ya katiba. Kutokana na michakato hii kuna dhana nyingi mpya ambazo hujitokeza. Dhana hizi kwa vile ni geni huwa vigumu kutafsiriwa. Tutaangalia jinsi dhana hizi zilivyotafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili na kuonyesha changamoto za kisimu zilizopo. Uwanja wa kutafsiri sheria kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili ni uwanja ambao bado haujatiliwa maanani sana. Ni mahitaji ya kikatiba kwamba lugha ya Kiswahili ni lugha rasmi nchini Kenya na kwa hivyo tafsiri nyingi zitafanywa hasa za kisheria kutoka lugha ya Kiingereza inayotumika kwa sasa kusawidi matini za kisheria hadi lugha ya Kiswahili. Tayari tafsiri ishatolewa ya katiba ya Kenya (2010). Hakuna tafsiri ambayo huwa imekamilika yaani ambayo haina dosari na ndio sababu utafiti wetu unahusu kuchunguza matatizo yanayoweza kuwa katika tafsiri ya katiba. Ni maoni yetu kuwakwa kufanya utafiti huu tutakuwa tumeweka wazi changamoto hizi na pia kuonyesha mikakati inayoweza kutumiwa kukabiliana na changamoto hizi.

1.3 Malengo ya utafiti

Utafiti wetu utaongozwa na malengo yafuatayo;

- (i) Kuchunguza changamoto za kiisimu za kutafsiri matini za kisheria kama zilivyo katika sura ya kumi na moja ya katiba ya Kenya.
- (ii) Kuchunguza ukosefu wa ulinganifu wa kiistilahi na athari zake katika sura ya kumi na moja ya katiba ya Kenya (2010).

1.4 Nadharia Tete

Utafiti wetu utaongozwa na nadharia tete zifuatazo;

- (i) Kwamba changamoto za kutafsiri matini za kisheria huwa za kiisimu hususan katika sura ya kumi na moja ya katiba ya Kenya (2010).
- (ii) Kwamba ukosefu wa ulinganifu wa kiistilahi unaleta athari ya upotoshi wa maana katika sura ya kumi na moja ya katiba ya Kenya (2010).

1.5 Sababu za kuchagua mada hii

Sababu yetu kuu ya kuchagua mada hii ni kuwa katiba ni stakabadhi muhimu kwa vile ndiyo sheria kuu nchini. Tafsiri mwafaka ya katiba inahitajika ili iweze kutumika sambamba na nakala ya Kiingereza. Watakaotumia nakala ya Kiswahili wanastahili kupata kwa ukamilifu yaliyo katika nakala asili. Kama tulivyokwisha kutaja, sura ya kumi na moja ya katiba ya Kenya (2010) inahusu ugatuzi. Ugatuzi ni dhana mpya nchini Kenya. Dhana hii mpya imeleta istilahi mpya ambazo lazima zitafsiriwe kwa usahihi ili kusiwe na dharuba za kiisimu na vilevile za kisheria. Serikali ya ugatuzi ni jambo ambalo linamhusu kila mwananchi wa Kenya. Tafsiri mwafaka ya sura hii itawanufaisha Wakenya wengi wanaotumia lugha ya Kiswahili kupata uelewa kuhusu masuala ya ugatuzi.

Kulingana na katiba kila stakabadhi rasmi, mawasiliano yote rasmi yatakayotolewa kwa lugha ya Kiingereza lazima yatolewe kwa lugha ya Kiswahili. Sababu nyingine ni kuwa hakuna utafiti mwingi uliofanywa kuhusu tafsiri za sheria za Lugha ya Kiswahili na hivyo hakuna makala rejelea ya kutosha kuhusu suala hili. Tukifanya utafiti huu tutakuwa tumechangia katika kukuza matini rejelea katika uwanja huu wa kiusomi. Kwa kufanya utafiti huu pia tunaamini kuwa tutakuwa tumeshughulikia changamoto za kutafsiri matini za kisheria na kuweka wazi mikakati ya kukabiliana na changamoto hizi. Ni maoni yetu kuwa utafiti huu utakuwa wa manufaa sana kwa wanaoshughulika na tafsiri za kisheria.

1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti wetu utajikita katika kuonyesha changamoto za kutafsiri matini za kisheria. Kwa vile uwanja wa kisheria ni mpana mno, tutachunguza changamoto hizi kama zinavyojitokeza katika katiba ya Kenya (2010). Katiba huwa na sura kumi na nane ambazo zimegawanywa katika vijisehemu kadhaa. Utafiti wetu utajikita katika sura ya kumi na moja inayohusu ugatuzi. Sura hii imegawanywa katika sehemu saba na ina vifungu ishirini na sita.

Katika utafiti wetu tutajishughulisha na kuonyesha changamoto za ukosefu wa ulinganifu wa kiistilahi katika tafsiri ya sura hii. Lengo letu si kutoa tafsiri mwafaka ya sura hii lakini ni kuithamini tu kama matini ya kisheria. Hata hivyo tutatoa mapendekezo yetu pale tutaona panafaa.

1.7 Msingi wa Nadharia

Utafiti wetu utaongozwa na nadharia ya *Skopos*. Nadharia hii iliasisiwa na Hans Vermeer (1978). Neno ‘*skopos*’ linatokana na neno la Kigiriki ambalo ni istilahi iliyo na maana ya nia ya kutafsiri. Kwa mujibu wa nadharia hii ya *Skopos* kutafsiri ni kutoa matini lengwa ambayo ina jukumu linalofaa kama ilivyo katika matini chanzi. Nadharia hii husisitiza kuwa, kimsingi kutafsiri kunafaa kushughulikia jukumu la matini chanzi na matini lengwa. *Skopos* huangalia kutafsiri kama kitendo kilicho na malengo au nia. Kitendo hicho kinafaa kumlenga mpokeaji katika mazingira ya tafsiri hiyo. Kulingana na nadharia hii, kutafsiri ni kuzalisha matini lengwa, kwa lengo lengwa na mpokezi lengwa katika mazingira lengwa.

Jukumu la tafsiri hutegemea ujuzi, matarajio, maadili na kaida za wasomaji lengwa ambao nao huathiriwa na hali na utamaduni wao. Nadharia hii hutilia maanani utamaduni wa wasomaji wa matini lengwa na jukumu ambalo matini itatekeleza katika utamaduni wa wasomaji hao. Kutafsiri huonekana sio tu kama mchakato wa kuhamisha msimbo, lakini kama umbo maalum la tendo la binadamu. Kama tendo lingine lolote la binadamu, kutafsiri huwa na nia. Ni juu ya mtafsiri kuamua ni jukumu gani matini chanzi itatekeleza katika kazi ya tafsiri. Matini lengwa yaweza kufanyiwa mabadiliko kulingana na utamaduni lengwa lakini pia imfahamishe msomaji kuhusu utamaduni chanzi. Kulingana na Vermeer (1989: 82) “hakuna matini chanzi iliyo na tafsiri moja tu ambayo ni sahihi na inayokubalika”. Hivyo basi kila tafsiri lazima itangaze *Skopos* yake – yaani ieleze nia yake. *Skopos* ya matini lengwa sio lazima ifanane na *Skopos* ya matini chanzi. Ni lazima nia au *Skopos* ya matini lengwa ifafanuliwe ndiyo tafsiri itekelezwe.

Kuna wale wanaopinga nadharia hii kama vile Schreitmuller (1994), Koller (1990) na Chesterman (1994). Wanasema kuwa nadharia hii inaruhusu urekebishaji wa matini lengwa jambo linalofanya matini lengwa kutoaminika. Kulingana nao lazima kuwe na udhibiti wa marekebisho ya matini lengwa ili isitofautiane sana na matini chanzi. Wanazidi kusema kuwa hata kama tafsiri itatimiza nia (*Skopos*) yake vizuri, inaweza kuwa na upungufu katika nyanja zingine hasa katika uteuzi wa leksia, sintaksia au mtindo. Kwa upande mwingine, kuna wale wanaounga mkono nadharia hii kama vile Reiss (1990). Anasisitiza kuwa, mara tu mtu anapojua nia ya tafsiri, mikakati mingine kama vile urekebishaji na uundaji upya wa matini utajileta wenyewe wakati wa kutafsiri. Nadharia ya *Skopos* inasaidia kuangalia matini lengwa. Kama matini, tafsiri haibainishwi tu na matini chanzi lakini hubainishwa pia na nia yake.

Ingawa nadharia hii ya *Skopos* ina udhaifu wake, tunaona kuwa itatufaa sana katika utafiti wetu. Hii ni kwa sababu matini za kisheria huandikwa ili kutimiza lengo fulani la kisheria. Matini hizi huandikwa kwa lugha ya kisheria ambayo huwa vigumu kwa msomaji wa kawaida ambaye hana ujuzi wa kisheria kuelewa maana yake. Ikiwa mtafsiri atalenga kuweka matini kwa lugha halisi inayoweza kueleweka na msomaji lengwa kwa urahisi bila kupotosha maana, basi atakuwa amefanikiwa katika kutafsiri kwake. Kwa vile nadharia hii inasisitiza nia (*Skopos*) ya tafsiri, basi tutaitumia kama mwongozo wetu katika utafiti huu. Kipengele kimoja muhimu cha nadharia hii ni kuwa tafsiri hubainishwa na *skopos* yake yaani nia. Ili tafsiri iwe kamilifu lazima itimize nia iliyokusudiwa. Jambo la pili ni kuwa ML lazima iwe na ule ushikamano wa undani na vilevile iwe na mshikamano na MC. Tutatathmini iwapo vipengele hivi vya *skopos* vinadhihirika katika sura ya kumi na moja ya katiba.

1.8 Yalioandikwa Kuhusu Mada hii.

Kazi nyingi zimewahi kuandikwa kuhusu tafsiri kwa jumla. Nyingi za kazi hizi ni za kinadharia. Kazi hizi zitatusaidia katika kujenga msingi wa utafiti wetu. Mojawapo wa kazi hizi ni makala ya Jakobson (1959) ‘Vipengele vya kiisimu vya tafsiri’. Jakobson anaelezea kuhusu kutafsiri baina ya lugha mbili tofauti. Anaongozwa na nadharia ya lugha iliyoasisiwa na mwanaisimu Ferdinand de Saussure (1857-1913). Kama anavyonukuliwa na Jakobson, Saussure alibainisha kati ya kiashiria na kiashiriwa. Kulingana na Jakobson ni vigumu kupata maneno mawili kutoka lugha tofauti yanayofanana kile kinacholingana ni maana. Maoni haya ya Jakobson tutayatilia maanani hasa tutakapokuwa tukiangalia changamoto za ukosefu wa ulinganifu wa kiistilahi katika kutafsiri matani za kisheria.

Ali (1965) ameandika makala ‘Matatizo na Matatuzi ya kutafsiri Sheria’. Katika makala haya, Ali ameyajadili matatizo yanayomkabili mtafsiri wa sheria hasa anapotafsiri kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili. Matatizo haya ni pamoja na kuwepo kwa maneno mengi katika lugha ya Kiingereza ambayo huwa na maana fulani katika msemu wa kawaida na maana tofauti yanapoingizwa katika msemu wa kisheria. Tatizo la pili ni kuwepo kwa maneno mengi katika sheria ya Kiingereza yanayoeleza mawazo ambayo hayakuwa katika Kiswahili wala katika ustaarabu wa Kiswahili. Tatizo la mwisho ni kuwa kuna mawazo mengi ya kisheria ambayo hayana maneno katika hicho Kiingereza lakini yamechukuliwa maneno kutoka katika lugha nyingine. Ali pia amejadili matatuzi ya matatizo haya. Matatuzi haya ni kama vile kuchunga maana inayotakikana ya maneno kisheria, kubuni maneno mapya, kutoa maelezo ya maneno yasiyoweza kutafsiriwa kwa neno moja na kukopa maneno kutoka lugha zingine. Kwa hakika,

makala haya ya Ali yatatufaa sana kwani utafiti wetu unashabahiana na yaliyojadiliwa hapa.

Weston (1965), katika makala yake ya *'Law in Swahili- Problems in Developing National Language'* ameangazia matatizo ya kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya sheria nchini Tanzania. Amejadili changamoto za kiisimu ambazo watafsiri wa sheria walikabiliana nazo wakati wa kutafisiri sheria. Changamoto hizi ni kama vile kutafsiri kutoka kwa mfumo mmoja wa kisheria hadi mwingine, kujaribu kufuata kanuni ya neno moja tafsiri moja, yaani neno moja liwe na tafsiri moja pekee na kwamba istilahi nyingi zilikuwa zimeundwa kutokana na nahau za Kiingereza. Vilevile ameonyesha mikakati waliyotumia kukabiliana na changamoto hizi. Mikakati hii ni kama vile kunyambua maneno yaliyopo katika lugha ya Kiswahili ili kupata maneno zaidi, uundaji wa maneno, kutumia maneno ya kawaida na kuyapa maana za kisheria, kuumba maneno mapya ambayo hayakuwepo na kuchukua maneno ya kawaida katika lugha na kuyapa maana za kisheria, kutafsiri kwa njia ya maelezo na kukopa maneno kutoka lugha zingine. Vilevile alionyesha ufanisi walioweza kuupata katika harakati za kutafsiri Sheria. Ufanisi huu ni kuwa, japo kutafsiri sheria si jambo rahisi wataalamu waliweza kutafsiri matini za kisheria za kutumiwa katika mahakama za kimsingi na wakaweza kutafsiri matini zingine za sheria za nchi. Makala hii ya Weston ni ya thamani kubwa katika utafiti wetu kwa vile yatatuelekeza katika kutimiza malengo yetu ya utafiti.

Brower (1966) anasema kwamba tafsiri huonyesha hali ya maana na maana zinazolingana na kubainisha ni maana gani iliyopo katika usemi fulani. Anasisitiza kuwa mtafsiri hana budi kuelewa tamaduni za lugha hizi mbili. Katiba

ya Kenya (2010) ni zao la marekebisho ya katiba ya 1964. Katiba hii iliandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza ni lugha za tamaduni mbili tofauti. Hatutakuwa na budi kuelewa tofauti hizi za kitamaduni ili kuelewa vyema vile tofauti hizi zinavyochangia kuweko kwa changamoto. Dhana ya ugatuzi hutofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine. Nchini Uingereza dhana hii ni tofauti na ilivyo nchini Kenya. Kwa hivyo kuelewa tamaduni za lugha mbili zinazohusika kutatuwezesha kuelewa vyema changamoto za kutafsiri kama zinavyojitokeza.

Mtaalamu mwingine aliyeandika kuhusu nadharia za tafsiri ni Newmark (1982). Yeye amefafanua sababu zinazopelekea kuanzishwa kwa nadharia za tafsiri. Anasema kuwa sababu tatu kuu zinazopelekea kuanzishwa kwa nadharia za tafsiri ni kama vile wingi wa makosa katika tafsiri zilizochapishwa, pili ni kuwepo kwa idadi kubwa na inayozidi kuongezeka ya asasi zinazojishughulisha na kazi ya tafsiri, na tatu ni mfumuko wa istilahi katika taaluma mbalimbali, hasa sayansi na teknolojia na haja ya kusanifisha istilahi hizi ili kufanikisha tafsiri baina ya lugha moja na nyingine. Maoni haya ya Newmark yatajenga msingi wa nadharia utakaotuongoza katika utafiti wetu.

Baker (1992) anaangalia ulinganifu katika ngazi mbalimbali katika mchakato wa kutafsiri. Yeye anazingatia vipengele tofauti katika kutafsiri kwa kutumia mwelekeo wa kiisimu na ule wa mawasiliano. Anabainisha aina zifuatazo za ulinganifu. Kwanza ni ulinganifu unaotokea katika kiwango cha neno na unaotokea katika kiwango kilicho juu ya neno wakati wa kutafsiri kutoka lugha moja hadi nyingine. Neno ni kipashio cha chini kabisa kilicho na uwezo wa kubeba maana. Katika kutafsiri, neno linaweza kuangaliwa kwa njia mbili.

Kwanza neno laweza kuuangaliwa katika msingi wa umbo. Neno huangaliwa kama limeumbika kutokana na vipashio vingi au kama limeumbika kama mofimu huru. Neno vilevile huangaliwa kama lina maana moja au limesheheni maana nyingi. Katika kutafsiri, mtafsiri anafaa atathmini kama kuna ulinganifu wowote kati ya lugha chanzi na lugha lengwa kuhusiana na jinsi viambishi vinavyojitokeza. Ikumbukwe kuwa mofimu bali na kuonyesha maana huwa na majukumu mengine ya kisarufi kama vile kuonyesha njeo, wakati, hali, idadi au jinsia.

Jambo la pili ambalo Baker aliangalia ni ulinganifu wa kisarufi wakati unaporejelea tofauti za kategoria za kisarufi kutoka lugha moja hadi nyingine. Kanuni za kisarufi za leksia na sintaksia huzingatiwa. Kwa kuhakikisha kuna ulinganifu wa kisarufi maana ya matini chanzi huhifadhiwa. Aina ya tatu ni ulinganifu wa matini unaporejelea ulinganifu kati ya matini chanzi na matini lengwa ukizingatia ujumbe na mshikamano wa matini. Matini iliyotafsiriwa lazima iwe na mshikamano kama ile matini chanzi. Mwisho ni ulinganifu wa kipragmatiki ukizingatia maana hushisha. Baker anasema kuwa jukumu la mtafsiri ni kuumba upya kusudio la mwandishi katika utamaduni mwingine kwa njia itakayomwezesha msomaji wa matini lengwa kuielewa bila tatizo lolote.

Kazi nyingine muhimu ya tafsiri ya sheria ni ya Mlacha (1999). Mlacha aliandika kamusi ya sheria ya Kiingereza-Kiswahili. Hata kama kamusi hii haikushughulikia istilahi zote zinazopatikana katika sheria tutairejelea mara kwa mara katika utafiti wetu kupata tafsiri za maneno na istilahi.

Sakareva (2001) katika makala '*Difficulties and some Problems in Translating Legal Documents*', amefafanua baadhi ya matatizo ya kutafsiri matini za kisheria.

Matatizo haya ni kama vile kutafsiri kutoka kwa mfumo mmoja wa kisheria hadi mwingine, kuhamisha mawazo kutoka utamaduni wa mwandishi hadi utamaduni wa mpokeaji, ukosefu wa ulinganifu wa istilahi na utoshelevu katika matini za kisheria miongoni mwa changamoto zingine. Vilevile anaelezea sifa mahsusi za matini za kisheria na lugha ya sheria kwa jumla.

Gentzler (2001) amezungumzia kuhusu ulinganifu wa maana katika tafsiri. Anaangazia kazi ya Nida na kusema kuwa Nida alitumia misingi ya Chomsky ya umbo ndani na umbo nje ya tungo ili kuelezea maana. Mtazamo huu wa kiisimu utatusaidia sana tutakapokuwa tukichanganua maumbo kama yalivyotafsiriwa. Cao (2007) ameanisha matini za kisheria kwa njia mbalimbali na akaonyesha matatizo ya uainishaji huo. Amezungumzia kuhusu lugha ya kisheria na akaeleza sifa bainifu za sajili ya sheria. Amefafanua chanzo cha matatizo ya kutafsiri sheria katika viwango mbalimbali vya kiisimu.

1.9 Njia za utafiti

Tutatumia data za msingi na zile za upili katika utafiti wetu. Data za msingi tutazitoa moja kwa moja kutoka sura ya kumi na moja ya katiba. Data hizi zitabukia masuala ya kiisimu. Tutaangalia masuala haya katika ngazi zote za kiisimu yaani fonolojia, mofolojia, sintaksia na pragmatiki. Tutapata data hizi kwa kusoma katiba ya Kenya (2010). Tutasoma nakala ya Kiingereza na ya Kiswahili ili kulinganisha maana kama ilivyowasilishwa katika nakala hizi. Tutatathmini iwapo kuna upotoshi wa maana katika nakala ya Kiswahili. Tutatoa mifano ya tafsiri potovu kama zilivyo katika sura hii ya kumi na moja. Hatimaye tutachanganua mifano hii na kuiwasilisha kwa njia ya maelezo kuonyesha

changamoto za kiisimu za kutafsiri matini za kisheria. Vilevile tutatumia data hii kuonyesha mikakati iliyotumiwa kukabiliana na ukosefu wa ulinganifu wa maana.

Data za upili nazo tutazikusanya kwa kusoma maktabani. Tutajikita katika kusoma vitabu, tahakiki, makala na majarida mbalimbali kuhusu tafsiri kwa jumla na vilevile tafsiri za kisheria. Data hizi za upili tunazokusudia kukusanya zinahusu mambo ya kinadharia ya tafsiri kwa jumla, sifa za matini za kisheria na istilahi mbalimbali zinazotumiwa katika tafsiri na katika sheria. Data hizi tutazitumia katika kuchanganua data za kimsingi tulizopata kutoka kwa nakala za katiba.

SURA YA PILI

Ujumla na upekee wa Tafsiri za kisheria

2.0 Utangulizi

Katika sura hii tutaangalia ujumla na upekee wa tafsiri za kisheria. Kwanza tutaangalia mambo ya kijumla ya tafsiri. Mambo haya ni pamoja na; dhana ya tafsiri, dhima ya tafsiri na nadharia ya tafsiri. Pili tutaangalia matini za kisheria kwa jumla, sifa za matini hizi, changamoto za kutafsiri matini hizi kwa ujumla na mikakati inayotumiwa kukabiliana na changamoto hizi. Tatu tutashughulikia katiba kama matini ya kisheria. Tutachanganua sifa maalum za katiba na changamoto za kutafsiri zinazotokana na sifa hizi maalum za katiba.

2.1 Dhana ya Tafsiri

Kwa hakika tafsiri sio jambo geni. Maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisayansi tunayofurahia leo duniani yalitokana na juhudi za ugunduzi wa watu wa kale na yametufikia kwa njia ya tafsiri. Karne ya sasa, yaani karne ya 21 inajulikana kama karne ya tafsiri kutokana na wingi wa mfumuko wa kazi za tafsiri. Taaluma ya tafsiri imekua kwa kiasi kikubwa sana. Newmark (1988:5) anasema kuwa, “kutafsiri ni kutoa maana ya matini katika hali ambayo mwandishi alikusudia”. Hivyo kutafsiri ni kuhawilisha maana kutoka lugha moja hadi lugha nyingine.

Ili kufanikisha shughuli ya tafsiri ni lazima mambo mawili muhimu yazingatiwe, kwanza mawazo yanayoshughulikiwa sharti yawe katika maandishi na si vinginevyo na pili mawazo (au ujumbe) kati ya lugha chanzi na lugha lengwa sharti yalingane.

Kwa hakika, hakuna tafsiri iliyo sawa kabisa na matini chanzi. Ndiyo maana Catford (1965:20) anatumia kauli kuwa “mawazo yanayolingana na sio mawazo yaliyo sawa’. Hii ni kwa sababu tofauti za kiisimu, kitamaduni, kihistoria na kimazingira kati ya lugha hufanya iwe vigumu kutafsiri mawazo ya lugha moja bila kupoteza, kupotosha au kubadili maana hata kama ni kwa kiwango kidogo tu. Kazi kubwa ya mfasiri ni kujaribu kuleta ulinganifu mzuri kati ya matini chanzi na ile ya matini lengwa licha ya tofauti zisizoepukika. Hivyo basi tunaweza kusema kuwa tafsiri ni mchakato wa kuhamisha ujumbe ulioandikwa katika lugha chanzi hadi katika ujumbe ulioandikwa katika lugha lengwa kwa lengo la kutimiza ulinganifu wa maana. Nia ya mtafsiri iwe ni kutimiza ulinganifu wa maana kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo. Ulinganifu huu pia unaweza kuzingatiwa katika kiwango cha umbo na vilevile uamilifu wa matini lengwa. Ikiwa kuna uhusiano kamili wa umbo na uamilifu wa matini chanzi na matini lengwa, maana inayojitokeza itakuwa sahihi. Kama umbo tu ndilo lina uhusiano na hakuna uhusiano wa uamilifu basi maana itakuwa ni tata. Uhusiano wa uamilifu ukiwepo na umbo lisiwe muhimu, basi maana itakuwa sahihi. Ikiwa hakuna uhusiano wowote wa umbo na uamilifu wa lugha chanzi na lugha lengwa, hakutakuwa na maana yoyote yaani hakuna tafsiri iliyofanyika. Ufafanuzi huu unaweza kuelezewa vyema kwa kutumia jedwali lifuatalo.

Jedwali 1:1 Mahusiano ya umbo na uamilifu katika Tafsiri

Aina za mahusiano	Kielelezo cha aina.		
	Lugha chanzi	Lugha lengwa	Maana
1. Mahusiano ya umbo na uamilifu	umbo ↔ umbo uamilifu ↔ uamilifu	umbo uamilifu	Sahihi
2. Mahusiano ya umbo lakini sio ya uamilifu	umbo ↔ uamilifu uamilifu	uamilifu uamilifu	Sio sahihi/ni tata
3. Mahusiano ya uamilifu na sio ya umbo	Umbo uamilifu ↔ uamilifu	umbo uamilifu	Sahihi ikiwa umbo sio muhimu
4. Hakuna mahusiano ya umbo wala ya uamilifu	umbo uamilifu	umbo uamilifu	Hakuna maana yoyote (Nunge)

Kiini cha Jedwali-Beekman, J na Callow (1974).

2.2 Dhima ya Tafsiri

Dhima ya tafsiri katika maendeleo ya binadamu ni kubwa. Kwa kweli, tafsiri huunganisha jamii mbalimbali za watu wanaotumia lugha zinazotofautiana. Kwa mujibu wa Newmark (1988:7), tafsiri hutekeleza majukumu yafuatayo; Kwanza tafsiri ni njia ya mawasiliano. Tafsiri hutumika kama njia ya mawasiliano miongoni mwa mataifa mbalimbali. Hutumiwa kutolea maelezo ya kibiashara, maelekezo ya jinsi ya kutumia bidhaa zinazouzwa nchi za nje, hutumika kwenye vyombo vya habari miongoni mwa mengine. Ni muhimu tafsiri zifanywe kwa usahihi ili kufanikisha mawasiliano. Akisisitiza juu ya umuhimu wa tafsiri sahihi, Newmark amebaini kuwa mlipuko wa bomu la atomiki huko Hiroshima, Japan ulisababishwa na tafsiri tenge ya neno '*mokasutu*' lililotafsiriwa kwa makosa kuwa '*ignored*' badala ya '*considered*'. Pili tafsiri huwa kama nyenzo ya kueneza tamaduni za mataifa tofauti tofauti kwa mfano utamaduni wa Kirumi uliathiriwa sana na utamaduni wa Kiyunani kutokana na tafsiri.

Tafsiri pia huwa kama mbinu ya kujifunza lugha. Mazoezi ya kutafsiri humfanya mtu asome kwa undani na makini zaidi vipengee anuai vya kiisimu vya lugha anayotafsiri ili aweze kutoa tafsiri bora inayokubalika. Tatu, tafsiri huwa kama kiliwazo cha nafsi ya mtafsiri. Tafsiri humfanya mtafsiri aburudike na kuridhisha nafsi yake kadiri anavyotatua matatizo yake ya kifasiri. Tafsiri vilevile ni mbinu maridhawa ya kuhamisha maarifa na ujuzi. Maarifa kote ulimwenguni huguduliwa na jamii moja, halafu jamii hiyo huyahamisha kwa jamii nyingine kupitia tafsiri. Mfano mzuri ni ujifunzaji wa kutumia vyombo mbalimbali vya kisayansi kama

vile kutumia tarakilishi umefikia WanaAfrika Mashariki kupitia tafsiri ya vitabu vya Kiingereza.

Aidha maarifa na maoni ya watu kama vile Plato na Aristotle yameenea ulimwenguni kote kupitia tafsiri ya vitabu mbalimbali. Kupitia kwa tafsiri ya Kiswahili ya sura ya kumi na moja ya katiba, Wakenya wengi wasiomudu lugha ya Kiingereza wataweza kujisomea kuhusu suala la ugatuzi na hivyo kuweza kufanya uamuzi wao.

2.3 Nadharia za Tafsiri

Nadharia za tafsiri ndizo msingi wa kazi zote za kifasiri. Ni maelekezo juu ya vipengele anuai vya kifasiri vinavyopaswa kuzingatiwa katika kazi ya kufasiri. Nadharia za tafsiri huchunguza mbinu zinazofaa kutumika kufasiri kwa ufanisi matini ya aina fulani mahsusi. Dhima muhimu ya nadharia za tafsiri ni kuonyesha mbinu za tafsiri zinazofaa kutumiwa kufasiria aina nyingi mbalimbali za matini. Vilevile nadharia hutoa msingi, kanuni, sheria na vidokezo vya kufasiri matini na kuhakiki tafsiri, yaani matini zilizokwisha tafsiriwa. Nadharia pia huelekeza jinsi ya kushughulikia vipengee vidogovidogo kama vile maana na umuhimu wa vistari, italiki na makosa ya tahajia. Zifuatazo ni sababu tatu kuu zinazopelekea kuanzishwa kwa nadharia za tafsiri.

(a) Wengi wa makosa (ya kimuundo, kimaumbo na kimsamiati) katika tafsiri zilizokwisha chapishwa. Ni nadra sana kupata tafsiri nzuri zisizo na makosa.

(b) Kuwepo kwa idadi kubwa na inayozidi kuongezeka ya asasi zinazojishughulisha na kazi ya tafsiri.

(c) Mfumko wa istilahi katika taaluma mbalimbali, hasa sayansi na teknolojia na haja ya kuzisanifisha ili kuwezesha tafsiri baina ya lugha moja na nyingine kufanyika kwa ufanisi zaidi.

Nadharia za tafsiri ni jumla ya maarifa yaliyopo na yatakayopatikana kuhusu mchakato wa kutafsiri. Nadharia hushughulikia mambo manne yafuatayo katika mpangilio wake. Kwanza ni kubaini na kufasili tatizo la tafsiri. Kama hakuna tatizo la tafsiri, basi hapatakuwepo na nadharia ya tafsiri. Pili ni kuonyesha vipengee vyote vinavyopaswa kuzingatiwa katika utatuzi wa tatizo la tafsiri lililobainishwa. Tatu ni kuorodhesha taratibu au njia zote zinazowezekana kufanikisha tafsiri inayohusika. Na mwisho ni kupendekeza taratibu zinazofaa zaidi kutekeleza zoezi la kutafsiri pamoja na mbinu zilizo mwafaka zaidi kwa matini mahsusi inayoshughulikiwa.

Nadharia za tafsiri humsaidia mtafsiri afanye uteuzi mzuri wa kile kinachomfaa katika kutekeleza kwa ufanisi wa shughuli yake ya kufasiri. Nadharia haitakuwa na maana yoyote iwapo haitokani na matatizo ya kifasiri. Kunazo nadharia nyingi za tafsiri. Katika utafiti wetu tutaongozwa na nadharia ya *Skopos*. Kama tulivyokwisha eleza nadharia hii huchukulia kuwa tafsiri hufanywa kutekeleza nia fulani. Nia ya kutafsiri katiba ya Kenya (2010) ilikuwa kuweza kuwafikia wananchi wengi ili waweza kufanya uamuzi wao kuhusu kupitia kwa kura ya maoni. Vilevile lugha ya Kiswahili ni lugha rasmi nchini Kenya na hivyo ni lazima kila stakabadhi muhimu itolewa kwa lugha ya Kiswahili.

2.4 Uainishaji wa Matini za Kisheria

Uwanja wa sheria ni mpana mno. Hii ni kwa sababu nyanja zote za shughuli za binadamu, kwa kiasi fulani huwa zimezingirwa na sheria. Kwa sababu ya upana

huu wa uwanja wa sheria kunazo aina nyingi za matini za kisheria. Matini hizi hutofautiana kwa hali moja au nyingine. Matini hizi zinaweza kuainishwa kulingana na matumizi yake. Matini za kisheria zinaweza kuwekwa katika kategoria tatu kuu. Kategoria hizi ni; Matini elekezi kwa mfano sheria za nchi, mikataba , kanuni na mifumo inayokubalika, matini fafanuzi kama vile kazi za kiusomi zinazoandikwa kama vitabu vya kisheria; na matini elekezi-fafanuzi kwa mfano maamuzi ya mahakama, kandarasi na maelezo ya korti.

Kutokana na aina hizi tofauti za matini za kisheria tunapata aina tofauti za tafsiri za sheria. Kwanza ni tafsiri za sheria kwa lengo la kusanifisha. Matini za kisheria zilizotafsiriwa kwa lengo la kusanifisha huwa na ulinganifu halisi katika lugha mbili au zaidi. Matini hizi ni kama vile tafsiri za sheria ambazo kwanza husawidiwa katika lugha moja na baadaye hutafsiriwa katika lugha nyingine moja au zaidi kwa mfano sheria za nchi , katiba , mikataba n.k. Katika kategoria hii, lengo la kuwasiliana katika lugha chanzi na lugha lengwa hufanana. Kategoria ya pili ni kutafsiri sheria kwa kusudi la kuarifu. Tafsiri hizi ni pamoja na tafsiri za maamuzi ya korti, kazi za kiusomi , amri za serikali na matini zingine za kisheria ambazo tafsiri yake hulenga kupasha ujumbe kwa wasomaji lengwa. Aina hizi za tafsiri ni tofauti na za kategoria ya kwanza kwa vile hazifungi kisheria. Katika kategoria hii matini zilizo katika lugha chanzi ndizo hutekelezwa kisheria. Kategoria ya mwisho ni tafsiri za kisheria kwa kusudi la kijumla la kisheria au la mahakama . Kimsingi, tafsiri hizi huwa za kutoa ujumbe na huwa fafanuzi. Huwa ni aina za matini zilizotafsiriwa ili zitumike katika maendeleo ya mahakama kwa mfano ushahidi ulioandikwa. Aina hizi za tafsiri hutumiwa sana sana na wateja ambao hawazungumzi lugha inayotumika kortini. Matini asili katika kategoria hii ni kama vile mikataba, stakabadhi za kibinafsi, maelezo ya

mashahidi n.k. Ni kutokana na ni aina gani ya tafsiri ambayo inashughulikiwa inayomfanya mtafsiri kuamua atatumia njia gani ya kutafsiri. Njia hizi za kutafsiri ni kama vile tafsiri huru, tafsiri mawasiliano na tafsiri maana.

Tafsiri huru ambayo pia hujulikana kama tafsiri ya neno kwa neno ni aina ya tafsiri ambapo maneno hutafsiriwa bila kuzingatia kanuni za kisarufi, muktadha wala utamaduni wa lugha lengwa. Mpangilio wa mofimu wa lugha chanzi hubakia vilevile yaani haubadiliki. Aina hii ya tafsiri hujikita katika kutafsiri maana za kimsingi za mofimu na maneno na haijishughulishi na maana nyongeza au matilaba. Ni aina ya tafsiri ambayo husisitiza kufikishwa kwa kile kilicho katika makala inayotafsiriwa katika makala ya lugha pokezi kama kilivyo katika lugha ya makala.

Tafsiri mawasiliano ni aina ya tafsiri ambayo hutoa tafsiri ya tungo au usemi kwa kuzingatia kanuni za kisarufi, muktadha na utamaduni wa lugha lengwa. Tafsiri hii humlenga msomaji wa matini lengwa ambaye hatarajii kupata ugumu wowote katika matini atakayosoma, yeye hutarajia tafsiri nyepesi ya dhana za kigeni katika utamaduni wa lugha yake. Mtafsiri huwa huru kutafuta maneno au mafungu ya maneno yanayolingana na nahau, misemo, methali, utamaduni na mazingira ya lugha lengwa. Lengo la kutafsiri katiba ya Kenya lilikuwa kumfikia mwananchi wa kawaida ili aweze kufanya uamuzi wake. Lugha iliyohitajika ni nyepesi ili mwananchi asitatizike wakati wa kusoma nakala hii.

Tafsiri maana ni aina ya tafsiri ambayo huegemea sana kwenye lugha chanzi, yaani kwa mwandishi. Hulenga kutoa maana lengwa ya kila neno katika tungo kwa kuzingatia kanuni za kisarufi na za muktadha wa lugha lengwa.

Tafsiri maana huweka mkazo kwenye maana ya matini kama ilivyokusudiwa na mwandishi. Masahihisho ya kinachofikiriwa kimepotoshwa au uboreshaji wa aina yoyote (wa matini chanzi) havina nafasi katika tafsiri maana. Kila kipashio au neno katika matini chanzi lazima kitafsiriwe. Aidha kila dhana huelezwa kwa neno mahususi jambo ambalo hupelekea kwenye tafsiri fafanuzi. Aina hii ya tafsiri huwa kavu, ndefu na haizingatii utamaduni wa lugha lengwa. Katika kutafsiri matini za kisheria, maana haipaswi kupotoshwa kamwe na inafaa kufikishwa kama ilivyo katika lugha asilia. Mtafsiri anaweza kutumia njia zote tatu za kutafsiri katika tafsiri moja. Hata hivyo tafsiri maana ndiyo hutumika zaidi katika matini elezi kama vile nyaraka za kisheria. Kwa hivyo kwa maoni yetu, aina hii ya tafsiri ndiyo inafaa zaidi katika kutafsiri matini za kisheria.

2.5 Sifa za Kijumla za Matini za Kisheria

Mchakato wa kutafsiri sheria huwa changamano na mgumu kwa vile huhusiana na uhalisi wa sheria, lugha inayotumiwa katika sheria, tofauti za kitamaduni za lugha husika na tofauti za kiisimu. Mambo haya hufanya uwanja wa sheria kuwa na sifa za upekee unaopatikana tu katika sheria. Sifa hizi zinaweza kubainishwa kama sifa za kiisimu na zisizo za kiisimu.

Kwa jumla lugha ya sheria hutambulishwa na hali ya matumizi ya lugha sanifu, lugha tendaji na lugha ya kiufundi. Vilevile lugha inayotumika katika sheria huwa si wazi. Hii ni kwa sababu ya matumizi ya maneno ya kawaida lakini maneno haya huwa na maana za kisheria. Hali hii huhitaji msomaji wa matini za kisheria awe na uelewa wa kisheria ili kuweza kubaini kinachorejelewa. Lugha sanifu ya sheria ni lugha ambayo huhusishwa uumbaji wa kanuni, kuzalisha kanuni hizi na kuzionyesha kanuni hizo, yaani ni lugha elekezi. Sheria huwa na

jukumu la kimsingi katika jamii la kuongoza tabia za watu na kudhibiti mahusiano yao . Ili kufikia lengo hili, sheria hutumia lugha elekezi, fafanuzi na ya kuamuru. Lugha hii elekezi hufanya matini za kisheria kuwa na matumizi mengi ya mipaka na masharti. Kwa mfano, Kifungu 131 (2) (a) cha Katiba ya Kenya;

‘Rais ataiheshimu, kuifuata na kuilinda katiba’.

Sifa ya pili ya lugha ya sheria ni kuwa ni lugha tendaji au lugha tekelezi. Sheria hutumia lugha kutenda. Matokeo ya kisheria na athari za kisheria hupatikana kwa kutamkwa kwa maneno fulani. Kwa mfano ‘una hatia’; ‘utafungwa miezi sita’ n.k. Sheria pia hutumia lugha kueleza kwa mfano lugha inayotumika katika katiba ni lugha elezi. Sheria hutumia lugha kutenda kwa mfano mawaziri hutumia lugha kula kiapo. Kwa mfano

“Nitatekeleza majukumu yangu yote kwa mujibu wa sheria.....”

Lugha ya sheria huwa ya kiufundi. Hii ina maana kuwa sheria hutumia maneno ya kawaida lakini yenye maana maalum yanapotumiwa katika muktadha wa sheria. Kwa hivyo istilahi fulani zinapotumiwa katika sheria huwa na maana tofauti na zile zilizo katika matumizi ya miktadha isiyo ya kisheria. Sheria hutumia maneno ambayo huwa na maana fulani katika msemu wa kawaida na maneno yayo hayo yanakuwa na maana nyingine tofauti yanapoigizwa katika msemu wa sheria . Kwa mfano neno ‘Bill’. Neno hili katika kamusi za Kiingereza huwa na maana kama hizi zifuatazo katika lugha ya kawaida; (i) Namna fulani ya mdomo wa ndege, (ii) namna ya upanga, (iii) namna ya mundu (iv) sururu (v) ncha moja ya nanga ya makombe, lakini katika lugha ya kisheria lina maana ya, waraka, hati ya malamiko au maandishi yaliyo katika kina cha mswada wa sheria. Neno hili hubadilika maana yake katika sheria kwa kufuata ni kitu gani kimeongezwa. Kwa mfano,

ikiwa ni neno *exchange* limeongezwa na kuwa '*bill of exchange*' huwa na maana ya hawala lakini ikiwa ni '*bill of lading*' inakuwa hati ya upakizi. Hali hii ya kutofautiana maana ya maneno katika msemu wa kawaida na katika sheria imefanya lugha ya sheria iwe ngumu. Na ndipo ikawa sheria ni taaluma inayojitegemea yenyewe.

Si rahisi kuelewa bila kuisomea. Sheria pia hutumia lugha isiyo wazi. Lugha inayotumiwa katika sheria huwa tata na huhitaji ufafanuzi mwingi wa kisheria ili kuweka wazi kinachozungumziwa.

Kando na sifa hizi, kuna pia sifa za kiisimu za lugha ya sheria. Sifa hizi zinaweza kubainishwa kama sifa za kileksia, kisintaksia, kipragmatiki na kimtindo. Sifa moja bainifu ya kileksia ya lugha ya sheria ni msamiati changamano na wa kipekee unaopatikana katika lugha tofauti za kisheria. Sifa hii ya kiisimu ndiyo huonekana sana katika lugha ya kisheria kama lugha ya kiufundi. Msamiati wa kisheria katika kila lugha huwa mpana mno. Kwa sababu ya tofauti za mifumo ya kisheria, istilahi nyingi za kisheria katika lugha moja haziambatani na istilahi katika lugha nyingine. Sifa hii huleta tatizo la ulinganifu wa kiistilahi jambo ambalo huwa tatizo kubwa katika kutafsiri. Katika kila msamiati wa kisheria kuna upekee ambao haulingani katika lugha tofauti za kisheria. Kwa mfano, katika lugha ya kisheria ya Kiingereza, lugha huwa imejaa maneno ya kale kama vile '*thou*' na '*witnesseth*', maneno rasmi na yanayotumiwa kwa utaratibu fulani, mkururu wa maneno na maneno ya kawaida lakini yaliyo na maana zisizo za kawaida. Sifa muhimu ya sintaksia ya lugha ya sheria ni mtindo wa uandishi ulio rasmi na usiohusishwa na mtu maalumu. Kuna upekee wa kisintaksia katika kila lugha ya sheria. Kwa mfano, Kiingereza hutumia miundo changamani, usemi taarifa, vishazi vihusishi na

hutumia vikanushi vingi. Hivyo unapotafsiri kutoka lugha moja hadi nyingine iliyo na miundo tofauti ya kisintaksia lazima kutakuwa na changamoto.

Lugha ya sheria huwa na matumizi ya maneno ya kawaida lakini yaliyo na maana zisizo za kawaida. Hii ni sifa muhimu ya kisemantiki ya lugha hii ya sheria. Pia lugha hii huwa si wazi na kwa hivyo huleta utata katika kubaini maana hasa kwa wale wasio katika uwanja wa kisheria. Watafsiri wengi wa matini za kisheria huwa ni wanaisimu na sio wanasheria. Jambo hili huwa ni changamoto katika tafsiri zao.

Sifa ya kipragmatiki ni sifa nyingine ya kiisimu inayoathiri tafsiri za kisheria. Usemi wa kisheria hutenda vitendo. Maneno katika lugha ya kisheria hutofautiana katika maana na huwa na athari tofauti kutegemea ni nani ameyasema, ameyasemea wapi na ameyasema lini. Katika usemi tendaji, sifa kuu ya kiisimu inayojitokeza ni matumizi ya kila mara ya maneno ya kiutendaji kama vile, *'may'* na *'shall'* ambayo hutumika kwa wingi katika Kiingereza. Maneno haya yanapotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili huenda yasitoe kabisa dhana hiyo kama inavyojitokeza katika lugha ya Kiingereza. Jambo jingine la kuzingatiwa la kipragmatiki ni utata, uso dhahiri na shaka zinazopatikana katika matini za kisheria. Kauli zingine za kisheria huhitaji ufafanuzi wa kisheria ili kuelewa kinachomaanishwa. Uandishi wa kisheria hubainishwa na mtindo wa kitobinafsi na matumizi mapana ya sentensi tangazi ambazo hutangaza haki na wajibu. Mtindo wa kisheria huhusisha vipengele vya kiisimu vya lugha ya kisheria iliyoandikwa na vilevile jinsi ambavyo matatizo ya kisheria hutazamwa, huendeshwa na kusuluhishwa. Sifa hizi zote za kiisimu hufanya uelewa wa matini za kisheria kuwa mgumu kwa wasomaji wa kawaida wakiwemo watafsiri.

Sifa nyingine ambayo huathiri tafsiri za kisheria ni tofauti za mifumo ya kisheria. Kwa sababu ya tofauti za mifumo ya kisheria, istilahi nyingi za kisheria katika lugha moja huwa haziambatani na istilahi katika lugha nyingine. Hili huleta tatizo la ulinganifu wa kiistilahi ambalo huwa tatizo kubwa katika kutafsiri. Katika kila msamiati wa kisheria kuna upekee ambao haulingani katika lugha tofauti za kisheria. Kwa mfano, lugha ya kisheria ya Kiingereza huwa na sifa zifuatazo za kileksia.

(a) Hutumia istilahi za asili ya Kilatini na za Kifaransa. Kwa mfano, *bonafide*, *resjudicata* na *alibi* ambayo ni maneno ya Kilatini. Maneno yenye asili ya Kifaransa ni kama vile; *Contract*, *schedule* na *conditions*.

(b) Huwa na matumizi ya maneno ya kikale kwa mfano *inquire*, *peruse*, *forthwith* na *hereto*,

(c) Kuna matumizi ya kitenzi kisaidizi *shall* na *will*. Maneno haya wakati mwingine hutumiwa kwa njia ambayo huzua utata. Kwingine hutumiwa kuonyesha kuwa mtendaji wa kitendo kinachofuata kitenzi *shall* ana wajibu wa kukitekeleza kitendo hicho na kwingine kitenzi hiki *shall* kinapotumiwa humaanisha kuwa mtenda hana wajibu wowote wa kutekeleza kitendo fulani. Tazama mfano huu;

‘Wife shall have the right to retain her married name or shall also have the right to return to her maiden or former name’.

Matumizi ya *shall* katika sentensi hii hayana athari zozote za kisheria kwa Mtendaji yaani mtendaji hana wajibu wa kutekeleza yanayofuatwa na neno *shall*.

(d) Urudiaji wa maneno au uziada. Katika uandishi wa kisheria, Wasawidi hujaribu kuepuka kutumia anafora au viwakilishi virejeshi. Jambo hili ni muhimu kwa vile huzuia utata wa kimaana unaoweza kupatikana. Kwa mfano,

'the lessee shall pay the less or at the office of the lessor.'

Tukitumia kiwakilishi kimilikishi *his* badala ya neno *less or* katika kirai '*at the office of the lessor*' kutakuwa na utata wa ni wapi panaporejelewa. Kwa Mfano "*The lessee shall pay the lessor at his office*', itakuwa vigumu kuelewa ikiwa ni afisi ya *lessee* au ya *lessor* malipo yanafaa kufanyika.

(e) Matumizi ya lugha ya kiufundi. Haya ni maneno au vifungu vya maneno ambavyo hutumika katika taaluma ya kisheria pekee. Kuna yale ambayo ni ya kiufundi kabisa yaani hutumika katika uwanja wa kisheria pekee kwa mfano *decree, herein after, lease n.k.* na pia kuna istilahi ambazo ni maneno ya kawaida yanayotumiwa kila siku lakini yanapotumiwa katika sheria hupata maana mpya ya kisheria kwa mfano: *assignment, title, consideration n.k*

(f) Matumizi ya vitenzi-virai kama vile *putdown, write-off n.k.*

Sifa hizi za kileksia za lugha ya kisheria ya Kiingereza ndizo huleta matatizo wakati wa kutafsiri matini hizi kwa lugha ya Kiswahili.

Sentensi katika matini za kisheria huwa ndefu na changamani kuliko sentensi katika uandishi wa aina nyingine. Sentensi ndefu na changamani ni muhimu kwa sababu ya uchangamani wa masuala husika ya kisheria na mitazamio ya usawidi wa sheria. Pia masuala ya kisheria huhitaji ufafanuzi mwingi ili kuondoa utata unaoweza kupatikana. Vilevile kuna matumizi mapana ya masharti, mipaka na vikwazo. Hebu tutazame kifungu hiki cha maneno;'

'Mtu yeyote ambaye amri yoyote iliyotolewa chini ya fungu la 45 yatumika kwake akiona ameonewa na maagizo yoyote

yaliyotolewa katika amri hiyo anaweza wakati wowote kuchukua rufaani kwa maandishi kwa waziri’.

Kifungu hiki chote ni sentensi moja ndefu ambayo ni muhimu ili kutoa maana kamili ya kisheria iliyokusudiwa.

Uandishi wa kisheria hubainishwa na mtindo wa kitobinafsi, uandishi ulio rasmi usiohusishwa na mtu maalum. Kilicho tofauti ni kuwa matini tofauti za kisheria hutumia mtindo fulani maalum wa uandishi. Kwa mfano, mtindo unaotumika kuandika katiba ni tofauti sana na mtindo wa kuandika kandarasi.

Matini za kisheria pia huwa na urejeshi mwingi wa sheria zingine au vifungu vingine vya matini husika. Kwa mfano;

‘Panapotokea nafasi ya kazi katika afisi ya mwanachama wa Baraza la Kitaifa aliyechaguliwa chini ya Kifungu cha 97(1) (a) au (b).’

Kunazo sifa zingine ambazo si sifa za kiisimu lakini huathiri tafsiri za kisheria. Mojawapo wa sifa hizi ni tofauti za mfumo wa kisheria ya lugha chanzi na lugha lengwa. Mfumo wa kisheria hufungamana sana na utamaduni wa watu na historia yao. Dhana za kisheria, mila za kisheria na utekelezaji wa sheria hutofautiana kutegemea jamii husika. Kutafsiri sheria huwa kunahusu kutafsiri kutoka mfumo mmoja wa sheria hadi mwingine. Mfumo wa kisheria wa tusema wa Uingereza ni tofauti sana na mfumo wa kisheria wa Kiislamu au wa Waswahili.

2.6 Sifa za Katiba kama Matini ya Kisheria

Katiba ni sheria kuu katika nchi. Huwa ni seti ya kaida, kanuni na maadili ambayo huumba na kufafanua mipaka ya uwezo wa serikali na matawi yake. Katiba ni jumla ya kanuni ambazo kwazo huwezesha serikali kutawala.

Katiba ya Kenya (2010) ni zao la marekebisho ya katiba ya 1964. Katiba hii ina sura kumi na nane ambazo zimegawanya katika vijisehemu kadha. Uandishi wa katiba huwa chini ya usawidi wa kisheria. Huu ni uandishi wa kiufundi ambao hutumiwa na mawakili, mahakimu na watungaji wa sheria, na watu wengine walio kwenye uwanja wa kisheria kuelezea uchanganuzi wa kisheria, haki na majukumu ya kisheria. Katiba kama matini ya kisheria huwa na sifa mahususi ambazo huitofautisha na matini zingine za kisheria. Sifa hizi zinaweza kubainishwa kama sifa za kiisimu na vilevile sifa za kimtindo.

Sifa ya kwanza ya kimtindo ni kwamba katiba haundikwa kwa njia maalum. Katiba hupangwa katika sura mbalimbali ambazo huwa na anwani ya kile kilicho kwenye sura husika. Anwani hii huandikwa kwa herufi kubwa. Sura moja hugawanywa katika vijisehemu mbalimbali. Vijisehemu hivi huwa vimegawanya katika vifungu mbalimbali ambavyo hupewa nambari. Vifungu navyo huwa vimepangwa katika ibara mbalimbali ambazo huorodheshwa kwa kutumia nambari. Ikiwa ibara ina mambo kadhaa yanayoelezewa, mambo haya huorodheshwa kwa kutumia alfabeti.

Mfano wa sura ya katiba;

SURA YA KWANZA

MAMLAKA YA WANANCHI NA UKUU WA KATIBA HII

Mamlaka ya wananchi

1. (4) Mamlaka ya wananchi yanatekelezwa katika;

- a. Kiwango cha kitaifa; na
- b. Kiwango cha kaunti

Sifa ya pili ya katiba ni matumizi ya sentensi ndefu. Hii ni kwa sababu masharti na taratibu zilizo katika katiba lazima zielezwe kwa kina ili kusiwe na utata. Kwa mfano;

Kifungu 15(5) 'kifungu hiki kitatumika kwa mtu kuanzia tarehe ya kuanza kutumiwa kwa katiba hii, lakini mahitaji yoyote ambayo ni lazima yatimizwe kabla mtu anayestahili kusajiliwa kama raia, yatachukuliwa kama yaliyotimizwa pasi na kuzingatia iwapo mtu huyu aliyatimiza kabla au baada ya tarehe ya kuanza kutekelezwa kwa katiba hii au kiwango fulani kabla au baada ya tarehe ya kutekelezwa'.

Kifungu hiki chote ni sentensi moja ndefu. Sheria huhitaji maelezo mapana ambayo huwezekana kupitia matumizi ya sentensi ndefu. Urejelezi wa sehemu zingine za katiba ni sifa nyingine muhimu. Kwa mfano;

'Kifungu 17(2) Uraia wa mtu ambaye alichukuliwa kuwa raia katika kifungu cha 14(4) unaweza kupokonywa iwapo-'

Lugha ya katiba pia huwa imejaa masharti mengi na taratibu ambazo zinafaa kufuatwa. Hii ni kwa sababu dhima kuu ya katiba ni kuelekeza wananchi na pia kuonyesha mikapa na vikwazo vya serikali. Kwa mfano;

Kifungu (47) (1) *'kila mtu ana haki ya vitendo vya utawala ambavyo ni vya haraka, ufanisi, vya kisheria, vinavyofaa na sawa.'*

Kifungu 48: *'serikali itahakikisha uwezekano wa watu wote kufikia haki na malipo yoyote, yakihitajika yatakuwa ya kufaa na hayatazuia uwezekano wa kutendewa haki'.*

Sifa za kiisimu za katiba ni kama vile matumizi ya maneno ya kawaida lakini yaliyo na maana ya kisheria kwa mfano neno *provisions*, matumizi ya vitenzi-virai kama vile, *provides for, assumes office, holds office* nk. Katika matini za kisheria, kuna matumizi mengi ya vitenzi visaidizi *shall* na *will* na pia matumizi ya maneno ya asili ya Kilatini na Kifaransa kwa mfano, *ex officio, schedule* n.k. Katiba pia huwa na urudiaji mwingi wa maneno au uziada. Urudiaji huu husaidia kuepukana na utata unaoweza kutokea kama viwakilishi vingetumiwa. Mfano;

Kifungu 182 (2), *If a vacancy occurs in the office of county governor, the deputy county governor shall assume office as county governor for the remainder of the term of the county governor.*

Hapa maneno *'county governor'* yamerudiwa ili kuondoa utata. Sifa hizi za katiba huzua changamoto wakati wa kutafsiri.

2.7 Changamoto za Kutafsiri Matini za Kisheria

Mtu yeyote atakapokabiliwa na kutafsiri lugha moja kwa lugha nyingine huwa ameelekewa na jambo lisilokuwa rahisi. Hali hii kuzidi iwapo lugha ya Kiingereza ndiyo inayotafsiriwa katika Kiswahili. Mkanganyo huzidi endapo kinachotafsiriwa ni Kiingereza cha kisheria. Kwa kuwa lugha ya kisheria ni ngumu, kutafsiri sheria iliyoandikwa kwa Kiingereza katika Kiswahili huwa ni changamoto kubwa. Mojawapo ya changamoto hizi ni kupata istilahi za Kiswahili zinazolingana na istilahi zilizotumiwa katika Kiingereza. Ni jambo la kweli kuwa kuna mawazo mengi katika sheria ya Kiingereza yanayoelezea mawazo ambayo hayakuwapo katika Kiswahili wala katika ustaarabu wa Waswahili.

Ni wazi kuwa dhana isiyokuwepo katika utamaduni wa Kiswahili ni taabu kuwa na neno lake la Kiswahili. Si dhana tu bali pia vitu ambavyo vinavumbuliwa sasa huwa pia si rahisi kuvipatia majina kwa lugha nyingine isipokuwa ile ya taifa au kabila vumbuzi. Kwa mfano serekali ya ugatuzi ni dhana mpya nchini Kenya na kwa hivyo istilahi zingine hazina maneno ya lugha ya Kiswahili. Mifano ya istilahi hizi ni kama vile; *'governor'*, *'senator'* n.k. Ukosefu wa ulinganifu kiistilahi huleta ukosefu wa ulinganifu wa maana. Katika tafsiri za sheria, jambo la kwanza kubwa linalotakikana ni kuchunga maana inayotakikana ya maneno ya kisheria. Maneno ya kisheria huwa yana tafsiri maalum.

Neno la kisheria likiwa na maana fulani huwa maana nyingine fulani haiingii tena mahali hapo bila kuleta matatizo. Hali hii ya kuwa na mipaka katika maana ya maneno huleta ugumu mwingi katika kutafsiri sheria. Mfano mzuri wa kuonyesha mipaka ya sheria ni maneno *'Legal proceedings.'* Maneno haya yanaweza kutafsiriwa kama kesi. Ni kweli yana maana ya kesi lakini lakini hutokea wakati

mwingine ikawa '*legal proceedings*' limetumika bila ya kuwa na maana ya *kesi* kwa mfano mtu akienda mahakamani kuandikisha tuseme kandarasi, jambo hili laweza kuitwa '*legal proceedings*' lakini hapa halina maana ya *kesi*. Basi maneno '*legal proceedings*' yakipewa maana ya *kesi* tu peke yake yatakuwa yamepoteza maana ya pili. Kwa hivyo tafsiri inayofaa ni mashauri ya kisheria ambayo yanachanganya *kesi* na mashauri mengine yanayotaka yapitishwe katika mahakama.

Tatizo lingine linalopatikana katika kutoa maana ya maneno ya kisheria ya Kiswahili ni pale iwapo neno la Kiswahili linaeleza maana ya kisheria la Kiingereza na wakati huo neno hilo la Kiswahili lina maana nyingine ambayo kwa Kiingereza kuna neno lingine ambalo lina maana tofauti kabisa. Kwa mfano neno '*provisions*' linatafsiriwa kama masharti lakini neno hili masharti vilevile lina maana ya neno la Kiingereza '*terms*' na '*conditions*'. Maneno haya yana maana tofauti kabisa na neno '*provisions*'. Tatizo pia hutokea wakati wa kutafsiri maneno yaliyopewa maana ya kubuni. Maneno ya lugha huwa na maana yake au maana zake zilizowekewa kwayo. Ikiwa neno litapewa maana nyingine m'badala, basi maana hii itakuwa imebuniwa. Mtindo huu hutumika zaidi katika mambo ya elimu, sheria ikiwemo. Inapofika kutafsiri maneno yaliyopewa maana za kubuni, mtafsiri anaweza kutaabika. Ni lazima mtafsiri afahamu kama maana ya neno fulani ni maana halisi au maana buniwa.

Changamoto nyingine ya kutafsiri sheria ni kuhifadhi maana ya kisheria. Maana ya kisheria iliyopo katika msemu wa Kiingereza ni lazima ihifadhiwe na iwepo kwa ukamilifu katika Kiswahili. Ni rahisi pengine kufahamu kifungu cha maneno kina maana gani lakini si rahisi maana hiyo kutoa kwa ukamilifu, katika Kiswahili. Ni

vyepesi mno kuponyosha sehemu nyingine za maana unapoitia maana hiyo ya Kiingereza katika Kiswahili. Kiswahili na Kiingereza ni lugha mbili zilizo katika mifumo tofauti ya kisheria na vilivile tamaduni tofauti za kijamii. Totauti hizi huleta tofauti za mawazo. Waswahili wana mawazo ya namna yao na Waingereza vilevile huwa na mawazo ya namna yao. Ingawa mawazo haya yanaweza kutafsiriwa, pana ugumu kuweza kuyapatia tafsiri sawasawa. Kwani lugha yoyote inapotafsiriwa katika lugha nyingine ni taabu sana kuweza kuhamisha maana yote kwa ukamilifu na kuyatia katika hiyo lugha nyingine bila kupunguka hata kidogo. Jambo la maana kutazamwa ni kuwa ule upungufu wa maana usiwe mwingi hadi kugeuza sura ya maana asili.

2.8 Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto za Kutafsiri Matini za Kisheria

Licha ya kuwa kutafsiri matini za kisheria kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili huwa na changamoto, kunayo mikakati mbalimbali inayoweza kutumiwa ili kukabiliana na changamoto hizi. Njia mojawapo ni kutumia maneno yaliyopo katika Kiswahili. Hata kama kuna dhana ambazo hazikuwapo katika Kiswahili au ustaraabu wa Waswahili, kuna uwezekano wa kupata maneno katika Kiswahili ambayo yanaweza kutumiwa kuelezea maana ya dhana hizi. Maneno ya kawaida yanaweza kutumiwa katika sheria na kupewa maana nyingine ya kisheria. Vilevile kuna yale tayari yapo katika mfumo wa kisheria wa Kiislamu au wa sheria za kitamaduni. Mfano mzuri, ni maneno kama *'jurisdiction'* (mamlaka) *'testimony'* (ushahidi) na *'bill of exchange'* (hawala). Maneno ya Kiswahili yanaweza pia kunyambuliwa na kupata maana mpya. Kwa mfano *'sue'* au *'to claim'* ni dai. Kwa hivyo *'to claim against each other'* ni daiana na *'to cause claim against each other'* ni daianisha.

Njia zingine ambazo zinaweza kutumiwa ni; kukopa maneno kutoka lugha ya Kiingereza au lugha zingine na kuyapa maneno haya muundo wa Kiswahili. Kwa mfano,

governor- gavana,

county -kaunti,

speaker- spika

Vilevile unaweza kutafsiri kwa njia ya maelezo, hasa maneno ambayo si ya Kiswahili kwa mfano maneno kama *ex-officio* na *prima facie* yaweza kutafsiriwa kwa maelezo. Mkakati mwingine unaweza kutumiwa ni kuambatanisha maneno yaliyopo ili kuunda neno moja lenye maana mpya. Maneno yaliyopo kwenye lugha yanaweza pia kupewa maana nyingine mpya. Ie maana asilia huonekana kupotea au kusahaulika. Mtafsiri pia anaweza kutumia mbinu ya kubuni neno jipya kabisa na kulipa maana ya kisheria.

2.9 Hitimisho

Katika sura hii, tumejadili wasifu wa matini za kisheria kwa ujumla. Tumefanya hivi kwa kuonyesha sifa za kiisimu za lugha ya kisheria. Vilevile tumeelezea sifa zingine ambazo si za kiisimu lakini huathiri tafsiri za matini za kisheria. Kando na hayo tumejadili wasifu wa katiba na sifa maalumu za katiba kama matini yakisheria. Tumejadili pia changamoto za kutafsiri matini za kisheria na mikakati inayoweza kutumiwa kukabiliana na changamoto hizi. Kutokana na haya tumeona kuwa kutafsiri matini za kisheria ni jambo ambalo huwa na changamoto nyingi kwa sababu ya sifa maalum za lugha inayotumika katika sheria.

SURA YA TATU

Tathmini ya sura ya kumi na moja ya katiba ya Kenya (2010)

3.0 Utangulizi

Katika sura hii tutatoa ufafanuzi wa kijumla wa sura ya kumi na moja ya katiba. Kisha tutaorodhesha kwa kijumla dhana na istilahi zinazojitokeza katika sura hii kwa mfano dhana zinazohusiana na malengo, dhana zinazohusiana na miundo, dhana zinazohusiana na michakakato ya ugatuzi na dhana zinazohusiana na majukumu. Hatimaye tutawasilisha dhana na istilahi hizi kama zilivyotafsiriwa.

3.1 Ufafanuzi wa sura ya kumi na moja ya katiba

Sura ya kumi na moja ya katiba inahusu ugatuzi. Ugatuzi ni kile kitendo cha kupatiana mamlaka ya kisiasa kutoka serikali kuu hadi serikali za kiwango cha chini. Sura hii inahalalisha uumbaji wa kaunti arobaini na saba. Kila kaunti huwa na serikali yake kama ilivyoielezwa katika sheria ya serikali ya kaunti ya mwaka wa 2012. Sheria hii huwa huumba mifumo dhahiri ili kuhakikisha utekelezaji na ufanisi wa ugatuzi. Malengo ya sura hii ni kuweka wazi malengo ya ugatuzi, kanuni za serikali za ugatuzi, mamlaka na shughuli za serikali za kaunti, mipaka ya kaunti, mahusiano kati ya serikali ya kitaifa na zile za kaunti, kusimamishwa kwa muda kwa serikali za kaunti na mambo mengine ya kijumla ya ugatuzi. Kutokana na haya kunazo dhana ibuka na istilahi mpya zinazojitokeza. Dhana na istilahi hizi zimetumiwa kufafanua kuhusu ugatuzi na serikali ya ugatuzi. Sura hii imegawanywa katika vijisehemu saba. Tutaangalia dosari zilizopo katika sura hii. Tutafanya hivyo kwa kuziorodhesha dhana kama zinavyojitokeza katika MC na kuonyesha vile dhana hizi zimetafsiriwa katika ML.

3.2 Uwasilishaji wa Data kama ilivyo katika sura ya kumi na moja ya katiba

Katika sehemu hii tutatoa mifano ya tafsiri kama ilivyo moja kwa moja katika katiba. Tutaonyesha vile sehemu fulani kimeandikwa katika nakala ya Kiingereza na kufuatisha tafsiri yake kama ilivyo katika ML. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya tafsiri potovu.

MC

Part 1---Objects and principles of devolved government

174. The objects of the devolution of government are-

- (a) to promote democratic and accountable exercise of power;
- (c) to give powers of self-governance to the people and enhance the participation of the people in the exercise of the powers of the State and in making decisions affecting them;
- (f) to promote social and economic development and the provision of proximate, easily accessible services throughout Kenya;
- (i) to enhance checks and balances and the separation of powers.

ML

Sehemu ya 1---Malengo na kanuni za Serikali ya ugatuzi

174 Malengo ya serikali ya ugatuzi

- (a) kuhakikisha kuwa kuna mamlaka ya kidemokrasia na uwajibikaji wa serikali;

(c) kuwapa watu katika kila ngazi mamlaka ya kujitawala na kushiriki katika matumizi ya mamlaka ya Serikali katika kufanya maamuzi ya mambo yanayowaathiri;

(f) kustawisha miradi ya kijamii na kiuchumi na utoaji wa huduma za karibu na zilizo rahisi ili kumfikia kila mtu nchini Kenya;

(i) kuhakikisha kuna udhabiti na kugawana mamlaka kwa njia iliyo sawa.

MC

Part 2--- County governments

176. (1) There shall be a county government for each county, consisting of a county assembly and a county executive.

177. A county assembly consists of -----

(a) members elected by the registered voters of the wards, each ward constituting a single member constituency, on the same day as a general election of Members of Parliament, being the second Tuesday in August, in every fifth year;

(c) the number of members of marginalized groups, including persons with disabilities and the youth, prescribed by an Act of Parliament; and

(d) the Speaker, who is an ex officio member.

178 (3) Parliament shall enact legislation providing for the election and removal of speakers of the county assemblies.

Election of county governor and deputy county governor

180 (4) If two or more candidates are nominated, an election shall be held and the candidate who receives the greatest number of votes be declared elected.

(6) The Independent Electoral and Boundaries Commission shall not conduct a separate election for the deputy governor but shall declare the candidate nominated by the person who is elected county governor to have been elected as the deputy governor.

181 (2) Parliament shall enact legislation providing for the procedure of removal of a county governor on any of the grounds specified in clause (1).

182 (3) If a person assumes office as county governor under clause (2), the person shall be deemed for the purposes of Article 180 (7) ---

(a) to have served a full term as county governor if, at the date on which the person assumed office, more than two and a half years remain before the date of the next regularly scheduled election under Article 180 (1);

ML

Sehemu ya 2—Serikali ya Kaunti

176 (1) Kila kaunti itakuwa na Serikali itakayokuwa na bunge na baraza la Kaunti.

177 (1) Baraza la Kaunti lina wanachama wafuatao-

(a) wanachama waliochaguliwa na wapiga kura waliosajiliwa katika wadi, kila wadi ikijumuisha eneo moja la uwakilishi siku ile ya kupiga kura ya uchaguzi mkuu wa kuwachagua wabunge, itakayokuwa Jumane ya pili ya mwezi Agosti baada ya kila miaka mitano.

(c) idadi ya wanachama kutoka katika makundi yaliyotengwa, wakiwemo watu walemavu, jamii za watu wachache na vijana, kama ilivyopendekezwa katika Sheria ya Bunge;

(d) spika, asiye mwanachama rasmi.

178 (3) Baraza litatunga sheria itakayoruhusu kuchaguliwa na kuondolewa afisini kwa maspika wa mabaraza ya kaunti.

180 (4) Ikiwa wagombeaji kiti cha gavana wawili au zaidi watateuliwa, kura zitapigwa katika kaunti hiyo na mgombeaji atakayepata kura nyingi zaidi atatangazwa kuwa mshindi.

181 (2) Bunge litatunga sheria ya kutoa kanuni za kufuatwa kumuondoa gavana afisini kwa msingi wowote uliotajwa katika ibara ya (1)

182 (3) Iwapo mtu ataikalia afisi kwa mujibu wa ibara ya (2), kwa minajili ya kifungu cha 180 (7), mtu huyo atachukuliwa kuwa-

(a) amehudumu kipindi kizima cha gavana wa kaunti iwapo, kufikia tarehe mtu huyo alipoingia afisi hiyo, zaidi ya miaka miwili na nusu imesalia kabla ya tarehe ya uchaguzi mwingine ilivyo kawaida chini ya kifungu cha 180 (1)

MC

Part 3 Functions and powers of the county governments

Respective functions and powers of national and county governments

186 (2) A function or power that is conferred on more than one level of government is a function or power within the concurrent jurisdiction of each of those levels of governments.

187 (1) (b) the transfer of the function or power is not prohibited by the legislation under which it is to be performed or exercised.

(2) If a function or power is transferred from a government at one level to a government at the other level—

(a) arrangements shall be put in place to ensure that the resources necessary for the performance of the function or exercise of the power are transferred;

ML

Sehemu ya 3 –Mamlaka na shughuli za Kaunti

Mamlaka na majukumu mahsusi ya serikali za kaunti na kitaifa

186 (2) Jukumu linalopatikana katika zaidi ya ngazi moja ya Serikali ni jukumu lililo katika eneo zaidi ya moja la utawala la ngazi hizo za Serikali.

187 (b) kuhamishwa kwa mamlaka au majukumu kunaafikiana na sheria ambazo zinafungamana na utekelezaji wake.

(2) (a) mipango itafanywa ili kuhakikisha kwamba gharama za utekelezaji wa mamlaka au shughuli hiyo iliyohamishwa imefanikishwa;

MC

Part 4—The boundaries of counties

188(1) The boundaries of a county may be altered only by a resolution-

(b)(ii) the senate ,with the support of at least two-thirds of all of the county delegations

(2) (b) physical and human infrastructure;

ML

Sehemu ya 4-Mipaka ya Kaunti

188(1) Mipaka ya kaunti inaweza kubadilishwa kwa pendekezo tu –

(b) (ii) seneti ikiungwa mkono na angalau wawakilishi wa kaunti wasiopungua thuluthi mbili ya ujumbe wa kaunti.

(2) (b) miundo msingi na uhalisia wao.

MC

Part 5- Relationships between governments

Cooperation between national and county governments

189 (3) In any dispute between governments, the governments shall make every reasonable effort to settle the dispute, including by means of procedures provided under national legislation.

(4) National legislation shall provide procedures for settling inter-governmental disputes by alternative dispute resolution mechanisms, including negotiation, mediation and arbitration.

190 (3) Parliament shall, by legislation, provide for intervention by the national government if a county government-

(5) The legislation under clause (3) shall-

(d) provide for a process by which the Senate may bring the intervention by the national government to an end.

191 (3) The following are conditions referred to in clause (2) (a)-

(a) the national legislation provides for a matter that cannot be regulated effectively by legislation enacted by the individual counties;

(b) the national legislation provides for a matter that, to be dealt with effectively requires uniformity across the nation and the national legislation provides that uniformity by establishing-

ML

Sehemu ya 5- Mahusiano katika serikali

Ushirikiano wa serikali ya kitaifa na za kaunti

189 (3) Katika kutofautiana kokote kule kwa Serikali, Serikali inayohusika itafanya kila jitihada kutatua mzozo huo ikizingatia taratibu za kisheria kama zilivyo katika sheria ya taifa.

(4) Sheria ya kitaifa itatoa mwongozo na taratibu za kutatua mizozo kati ya Serikali kwa mbinu M'badala za kutatua mizozo zikiwemo kushauriana, kupatanisha na kusuluhisha.

190(3) Bunge litatunga sheria itakayoruhusu serikali ya kitaifa kuingilia serikali ya kaunti iwapo-

(5) Sheria inayotajwa katika Ibara ya (3)-

(d) kutoa utaratibu utakaowezesha seneti kuhusika vyema ili kumaliza au kutoa suluhu kwa matatizo hayo.

191(3) Masharti yanayotajwa katika ibara ya (2) (a) ni yafuatayo-

(a) sheria za kitaifa hushughulikia suala ambalo haliwezi kutatuliwa na sheria zilizotungwa na kaunti peke yake.

(b) sheria za kitaifa hushughulikia suala ambalo ili lishughulikiwe kikamilifu, linataka sheria ambazo ni sawa katika taifa zima.

MC

Part 6-Suspension of the county governments

192(2) A county government shall not be suspended under clause (1) (b) unless an independent commission of inquiry has investigated allegations against the county government, the president is satisfied that the allegations are justified and the Senate has authorized the suspension.

(5) A suspension under this Article shall not extend beyond a period of ninety days.

ML

Sehemu ya 6-Kusimamishwa kwa muda kwa Serikali za kaunti.

192(2) Serikali ya kaunti haitasimamashwa kwa muda kulingana na ibara ya (1) (b) hadi tume huru ifanye uchunguzi wa mashtaka yaliyowasilishwa dhidi yake, Rais wa taifa aridhike kwamba mashtaka ni ya haki na seneti imeyaidhinisha.

(5) kusimamishwa kwa muda katika kifungu hiki hakuwezi kuwa kwa zaidi ya siku tisini.

MC

Part7-General

195(2) For the purposes of clause (1), an assembly has the same powers as the High Court to-

(c) issue a commission or request to examine witnesses abroad.

County assembly gender balance and diversity

197 (1) Not more than two-thirds of the members of any county assembly or county executive committee shall be of the same gender.

200 (1) Parliament shall enact legislation providing for all matters necessary or convenient to give effect to this Chapter.

(2) In particular, provision may be made with respect to-

ML

Sehemu ya 7 –Jumla

195 (2) Kwa sababu ya ibara ya (1), baraza lina mamlaka sawa na Mahakama kuu ya–

(c) Kutafuta idhini ya kuwahoji mashahidi ng'ambo.

Usawa na tofauti za kijinsia katika baraza la kaunti.

197(1) Wanachama wa baraza lolote la kaunti au kamati ya mamlaka kuu ya kaunti, wasiwe zaidi ya thuluthi mbili katika jinsia moja.

200 (1) Bunge litatunga sheria katika masuala yote muhimu au ya lazima kuidhinisha utekelezaji wa Sura hii

(2) Hasa sheria inaweza kubuniwa ili iangazie-

3.3 Hitimisho

Katika sura hii, tumetoa mhutajari wa sura ya kumi na moja ya katiba ya Kenya 2010. Tumeona kuwa sura hii inahusu ugatuzi na michakato ya ugatuzi. Kunazo istilahi maalum zilizotumiwa kuelezea dhana hii ya ugatuzi.

Katika sehemu ya kwanza ya sura hii, malengo na kanuni ya serikali ya kaunti yameelezwa. Istilahi zinazotumiwa kuelezea malengo haya ni kama vile,

promote

foster

ensure

facilitate

recognize

protect

enhance

Vilevile kuna istilahi ambazo zinahusiana na miundo. Istilahi hizi ni kama vile;

County government

county assembly

county executive

executive committees

parliament

governor,

speaker,

ex-officio member n.k.

Kuna pia dhana ambazo zinahusiana na michakato ya ugatuzi. Dhana hizi ni kama vile;

become vacant

assumes office

provides for

provision of

provided

Tumeona kuwa kuna matatizo ya tafsiri yaliyo katika sura hii. Tumeorodhesha baadhi ya sehemu za sura hii na kuonyesha tafsiri zake kama zilivyo katika katiba. Tumepigia mstari pale tunaona kuwa pana tafsiri potovu. Tutachanganua mifano hii katika sura ya nne ili kuonyesha changamoto za kutafsiri matini za kisheria.

SURA YA NNE

Changamoto za kutafsiri matini za kisheria

4.0 Utangulizi

Katika sura hii, tutatumia mifano tuliyotoa katika sura ya tatu kuonyesha changamoto za kutafsiri matini za kisheria. Tutafanya hivyo kwa kuchanganua dhana na istilahi zinazohusiana na ugatuzi kadri zilivyotafsiriwa. Tutatumia vigezo vya kisimu vya Leksia, sintaksia na semantiki kuchanganua matatizo haya.

4.1 Ukosefu wa Ulinganifu wa Kiistilahi

Uibukaji wa dhana mpya huleta ukosefu wa ulinganifu wa kistilahi. Ukosefu wa ulinganifu wa kiistilahi huwa changamoto kubwa wakati wa kutafsiri matini za kisheria kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu ikiwa wazo halikuwa katika utamaduni wa Kiswahili ni taabu kuwa na neno lake la Kiswahili. Ukosefu huu wa ulinganifu wa kiistilahi huibua matatizo katika uwasilishaji wa maana. Katika kutafsiri matini za kisheria kutoka lugha moja au nyingine, maana lazima iwasilishwe kwa ukamilifu la sivyote kutakuwa na utata wa kufasili maana kisheria. Maana hukitwa katika mikitadha ya kileksia na kisintaksia. Tafsiri potovu za maneno zitajenga sentensi zisizo sahihi na huweza kuleta upotoshi wa maana. Ili tuweze kufafanua vyema jinsi ukosefu wa ulinganifu wa kiistilahi husababisha ukosefu wa ulinganifu wa maana, tutatumia mifano tuliyotoa katika sura ya tatu. Matatizo haya tutayachunguza katika ngazi za kisimu za kileksia, kisintaksia na kiseriantiki.

4.2 Matatizo ya kileksia

Lugha ya kisheria hutumia maneno ya kawaida lakini yaliyo na maana mahususi kisheria. Jambo la kwanza kubwa linalotakikana katika kutafsiri sheria ni kuchunga maana inayotakikana ya maneno ya kisheria. Maneno ya kisheria huwa yana tafsiri maalum. Neno la kisheria likiwa na maana fulani huwa maana nyingine fulani haiingii tena mahali hapo ili isilete matatizo juu ya kufahamu ni lipi lililokatazwa na ni lipi lililoamrisha au lipi litendwe na lipi lisitendwe, au lipi lifuatwe na lipi lisifuatwe. Hali hii ya kuwa na mipaka katika maana ya maneno huleta ugumu mwingi katika kutafsiri sheria. Katika kutafsiri sura ya kumi na moja ya katiba, jambo hili la kuzingatia mipaka ya maana za maneno halikufuatwa kwa ukamilifu.

Katika vifungu 174 (a) na 174 (h) maneno '*promote*' na '*enhance*', yametafsiriwa kama kuhakikisha. Kwa hakika maneno haya mawili tafsiri yake sio hakikisha. Vilevile maneno haya yana maana tofauti na kwa hivyo hayawezi kupewa tafsiri moja. Maana ya neno '*promote*' kulingana na kamusi ya Kiingereza lina maana ya kusaidia kitu kutendeka au kuendelea, nalo neno '*enhance*' lina maana ya kuongeza au kuzidisha ubora wa kitu. Maneno haya hayawezi kutafsiriwa kama hakikisha kwa vile neno hakikisha lina maana ya kuwa na uhakika wa jambo yaani kusadikisha jambo fulani. Tatizo lililopo ni kwamba kuna ukosefu wa istilahi ya Kiswahili inayolingana moja kwa moja na istilahi hizi '*promote*' na '*enhance*'. Ukosefu huu unaleta ukosefu wa ulinganifu wa kimaana.

Katika kifungu 174 (h) pia tuna istilahi '*checks*' and '*balances*'. Maneno haya yametafsiriwa kama kudhibiti. Tafsiri hii haitoshi kutoa maana kamili ya '*checks and balances*' kwani ni tata na tunabaki kuuliza ni kudhibiti kwa aina gani?

Maneno '*Checks and balances*' ni istilahi maalum katika sheria. Neno '*checks*' lina maana ya kanuni zilizobuniwa ili kudhibiti kiasi cha mamlaka hasa mamlaka ya kisiasa ya mtu mmoja au kikundi kimoja. Nalo neno '*balances*' lina maana ya hali ambapo nguvu za kisiasa hugawanywa kati ya makundi mbalimbali. Kwa hivyo tunaweza kusema kuwa '*checks*' na '*balances*' ni istilahi zinazotumika katika siasa kumaanisha taratibu za vyombo vya dola kudhibitiana ili kuzuia matumizi mabaya ya madaraka. Kutokana na maelezo haya basi, tafsiri kudhibiti haileti maana kamili ya '*checks and balances*'. Katika lugha ya Kiswahili hakuna istilahi linganifu ya '*checks and balances*'. Pengine mtafsiri angeendelea kuelezea kwamba ni kudhabiti kwa mamlaka.

Tatizo lingine linalojitokeza ni tafsiri ya maneno '*parliament*' na '*county assembly*'. Katika kifungu 178(3) neno '*parliament*' limetafsiriwa kama baraza na katika kifungu 181(2) limetafsiriwa kama bunge. Maneno '*county assemblies*' katika kifungu 178(3) yametafsiriwa kama mabaraza ya kaunti. Katika kifungu 176(1) si wazi kama tafsiri ya kifungu '*county assembly*' ni bunge la kaunti au baraza la kaunti. Tafsiri hizi zinakinzana na tunashindwa kufahamu ni dhana ipi inayowakilishwa hapa. Katika serikali ya ugatuzi '*parliament*' na '*county assembly*' ni mifumo miwili ya utawala ambayo ni tofauti. Mifumo hii hutekeleza majukumu tofauti. Viongozi waliochaguliwa katika '*parliament*' na katika '*county assemblies*' husimamia maeneo tofauti. Kwa sababu hii ni vyema mtafsiri angetoa tafsiri moja ya neno '*parliament*' na nyingine tofauti ya '*county assembly*' ili kuondoa utata wa kinachozungumziwa. Kisheria '*parliament*' ni kundi la watu waliochaguliwa kuunda na kubadilisha sheria za nchi. Watu hawa huwakilisha maeneo bunge kama yalivyofafanuliwa katika sheria za bunge 2012.

Nayo *'county assembly'* ni kundi la watu waliochaguliwa kukutana mara kwa mara kutengeneza sheria zinazohusu eneo fulani yaani kaunti. Kutokana na ufafanuzi huu wa kisheria, *'parliament'* jukumu lake ni kutunga sheria za nchi nzima tofauti na *'county assembly'* ambayo huwa na jukumu la kutunga sheria za eneo fulani yaani kaunti fulani. Kuchanganya tafsiri za maneno *'parliament'* na *'county assembly'* kunazua utata wa ni nini kinachozungumziwa. Atakayesoma tu tafsiri ya katiba hatajua kama kinachozungumziwa ni *'parliament'* au ni *'county assembly'*. Ni vyema kama neno *'parliament'* lingetafsiriwa kama bunge na *'county assembly'* lipewe tafsiri ya baraza la kaunti ili utata wa kinachowasilishwa usikuwepo. Iwapo mtafsiri atateua kutumia baraza kwa maana ya *'parliament'* basi litafsiriwe kwa ukamilifu kama baraza la kitaifa kwani *'parliament'* ni *'national assembly.'* Katika kifungu 176(1), pia kuna tafsiri potovu. Kifungu *'county assembly and a county executive'* kimetafsiriwa kama baraza na bunge la kaunti. Hapa hatuna uhakika ni maneno gani ambayo yametafsiriwa kama bunge la kaunti na ni yapi yaliyotafsiriwa kama baraza la kaunti. Ikiwa tafsiri ya *'County assembly'* ni baraza la kaunti, basi tafsiri ya *'county executive'* ni bunge la kaunti kulingana na kifungu hiki. Tafsiri hii sio sahihi kwa sababu *'county executive'* ni halmashauri kuu inayochaguliwa na baraza la kaunti kuendeleza shughuli za kaunti husika.

Vilevile tunalo neno *'function'* ambalo limetafsiri kwa njia mbili tofauti. Tukiangalia sehemu ya tatu, neno hili limetafsiriwa kama jukumu na vilevile kama shughuli. Ingawa maneno jukumu na shughuli yana maana zinazolingana, ingekuwa bora zaidi kama mtafsiri angechagua njia moja ya kutafsiri neno hili kwa vile neno hili limetumiwa katika muktadha sawa. Kulipa neno hili tafsiri zaidi ya moja kunaleta utata wa kimaana kwani msomaji lengwa huenda asibaini

kama maneno jukumu na shughuli yanarejelea kitu kimoja. Kwa maoni yetu neno jukumu linafaa zaidi kama tafsiri ya neno *function* katika muktadha huu.

Tatizo lingine linalojitokeza hapa ni katika kifungu 187(1). Hapa neno lilo hilo '*function*' lililo katika umoja limetafsiriwa kama majukumu. Neno majukumu liko katika wingi na kilicho katika matini chanzi ni '*function*' yaani jukumu moja tu.

Tafsiri ya vitenzi -virai ni tatizo lingine la kileksia ambalo linajitokeza. Lugha ya sheria huwa na matumizi mengi ya vitenzi -virai. Katika sura ya kumi na moja ya katiba kuna matumizi ya vitenzi -virai vifuatavyo;

assumes office

assumed office

provide for

provided for

shall provide

provides for

Providing for

Provision of

Katika kifungu 182, kifungu '*assumes office*' kimetafsiriwa kama atakalia ofisi nacho kifungu 182 (3), maneno '*assumed office*' yametafsiriwa kama alipoingia ofisi. Maneno '*assumes*' na '*assumed*' yametokana na mzizi mmoja wa kitenzi '*assume*'. Tofauti ni kwamba yako katika njeo tofauti neno '*assumes*' likiwa katika hali ya mazoea nalo '*assumed*' likiwa katika wakati uliopita. Kitenzi hiki '*assume*'

kimetafsiriwa kwa njia mbili tofauti kama **ingia** na **kalia**. Maneno kali na **ingia** yana maana tofauti kabisa. Vilevile maneno haya si tafsiri mwafaka ya neno ‘*assume*’ katika mktadha huu. Kwa hivyo kulitafsiri neno hili ‘*assume*’ kama kalia au ingia kunapotosha maana iliyokusudiwa katika matini chanzi. Tunaona kuwa neno ambalo lingefaa zaidi ni twaa kwa maana ya *assume*. Mfano mwingine wa tafsiri potovu ni katika kutafsiri vitenzi -virai *provide for, provided for, shall provide, provides for, providing for* na *provision*. Ingawa vitenzi hivi vimetokana na neno moja provide, vitenzi hivi vimepewa tafsiri zinazokinzana hasa ukiangalia muktadha wa matumizi. Katika kifungu 189 (3) maneno ‘*provided for*’ yametafsiriwa Kama, kama zilivyo. Katika Kifungu 189(4), maneno ‘*shall provide*’ yakatafsiriwa kama itatoa nacho kifungu 190(3) maneno ‘*provide for*’ yakatafsiriwa kama itakayoruhusu. Kifungu ‘*provides for*’ kimetafsiriwa kama hushughulikia katika kifungu 191(3). Maneno ‘*providing for*’ katika kifungu 200(1) yametafsiriwa kama katika. Neno ‘*provision*’ limetafsiriwa kama sheria katika kifungu 200(2). Tukiangalia mifano hii tunaona kuwa kuna ukosefu wa ulinganifu wa kiistilahi ambao huwa ni changamoto katika kutafsiri matini za kisheria. Tafsiri hizi zote hazileti maana kamili ya dhana hizi za kisheria. Kando na haya kunayo maneno mengine ambayo yana tafsiri potovu Maneno haya ni kama vile;

membership- wanachama

national legislation- sheria ya taifa

resources- gharama

foster- himiza

exercise of power- mamlaka

devolution of government - serikali ya ugatuzi.

Neno *membership* lingetafsiriwa kama uanachama na si wanachama kwani wanachama ni *members*. *National legislation* ni sheria ya kitaifa, *resources* ni rasilimali, *foster* litafsiriwe kama kukuza, *exercise of power* ni kutekeleza mamlaka na *devolution of government* ni ugatuzi wa serikali.

4.3 Matatizo ya Kisintaksia

Mtafsiri wa kisheria hutafsiri kutoka mfumo mmoja wa lugha (L.C) hadi mfumo wa pili (L.L). Mifumo tofauti ya lugha huwa na miundo tofauti ya sentensi. Kila lugha huwa na muundo wake wa sentensi unaokubalika. Huwezi ukalazimisha muundo wa lugha moja kwa mfano Kiingereza kwa lugha nyingine kama vile Kiswahili. Sintaksia ni kipengele kinachofaa kutiliwa maanani wakati wa kutafsiri. Kuvuruga muundo wa sentensi wa lugha fulani huleta matatizo ya kuelewa kinachowasilishwa yaani maana iliyotarajiwa haijitokezi waziwazi. Kwa hivyo, ni muhimu mtafsiri atilie maanani sintaksia ya lugha lengwa.

Katika sura ya kumi na moja ya katiba, tunayo matatizo ya kisintaksia yanayojitokeza. Matatizo haya yanaleta upotoshi wa maana ya matini lengwa. Kwa kawaida sentensi huundwa na maneno, hii ina maana kuwa tafsiri potovu za maneno zitaleta matatizo ya kisintaksia. Vilevile kutotafsiri maneno mengine yaliyo kwenye sentensi au kuongeza maneno ambayo hayakuwepo kutaleta matatizo ya kisintaksia. Ili kuchanganua vyema matatizo haya ya kisintaksia tutatoa mifano ifuatayo. Katika kifungu 174 (f) kifungu cha maneno “*easily accessible services throughout Kenya*’ kimetafsiriwa kama utoaji wa huduma za karibu zilizo rahisi kufikia kila mtu nchini Kenya. Tafsiri hii ina utata. Katika M.C

hakuna maneno na utoaji wa huduma za karibu yaliyopo ni “*easily accessible services*” yaani huduma zilozoz rahisi kufikiwa. Vilevile maneno kumfikia kila mtu nchini Kenya hayapo yaliyopo ni ‘*through out Kenya*’ yaani kote nchini Kenya. Kwa hivyo katika tafsiri hii tunaona mtafsiri alipachika maneno ambayo hayakuwepo katika M.C Ingawa kuongezea kwa maneno wakati mwingine hukubalika katika tafsiri, kuongeza huku katika mkutadha huu hakuhitajiki kwa vile kunaleta ukosefu wa ulinganifu wa maana wa M.C na M.L.

Mfano mwingine ni kifungu 188 (1). Katika tafsiri ya kifungu hiki, maneno ‘*county delegations*’ yametafsiri kama wawakilishi wa kaunti na vilevile ujumbe wa kaunti. Hakukuwa na haja ya kutumia tafsiri hizi mbili katika kifungu kimoja kwani ni urudiaji usio na maana yoyote. Neno ‘*delegations*’ laweza kutafsiriwa kama wawakilishi au wajumbe. Katika kifungu 177(1) (c) maneno ‘*including persons with disabilities and the youth*’ yametafsiriwa kama wakiwemo watu walemavu, jamii za watu wachache na vijana. Maneno jamii za watu wachache hayapo katika M.C kwani mtafsiri amekwisha tafsiri “*marginalized groups*” kama makundi yaliyotengwa. Kuongeza huku kwa maneno ambayo hayakuwepo katika M.C. kunaleta utata wa kimaana.

Katika sura hii ya kumi na moja ya katiba, kunayo maneno na hata vifungu vya maneno ambavyo havikutafsiriwa. Kuacha maneno na vifungu nje huleta utata wa kisemantiki. Wakati mwingine, mtafsiri hutumia mbinu ya kuacha nje maneno wakati wa kutafsiri hasa pale ambapo neno linakosa neno linganifu katika L.L. Kuacha huku kwa maneno nje hasa wakati wa kutafsiri matini za kisheria hakufai. Hii ni kwa sababu kila neno lazima litafsiriwe. Ikiwa hakuna neno mwafaka katika L.L, mtafsiri anaweza akatumia mbinu zingine kama vile kutafsiri kwa njia ya

maelezo. Katika kifungu 182 (3) maneno ‘*county governor*’ hayajatafsiriwa. Msomaji wa nakala ya Kiswahili hataelewa ni afisi gani inayorejelewa hapa tofauti na nakala ya Kiingereza ambapo jambo hili linajitokeza waziwazi kwamba ni afisi ya gavana wa kaunti. Kifungu 186 (2), mtafsiri hajatafsiri neno ‘*power*’. Neno ambalo limetafsiriwa ni ‘*function*’ ambalo limetafsiriwa kama jukumu. Tafsiri hii ni pungufu kwa vile ‘*function*’ na ‘*power*’ ni maneno yanayoashiria mambo mawili tofauti. ML basi haijawasilisha maana kamili kama ilivyo katika MC. Kwingineko ni katika kifungu cha 195(2). Hapa maneno ‘*issue a commission*’ hayajatafsiriwa kabisa. Vilevile kifungu 180(6) hakijatafsiriwa kabisa. Kuucha kifungu hiki ni balaa kisheria. Kutotafisiriwa kwa kifungu hiki chote kuna mfanya msomaji wa ML kutopata kwa ukamilifu yaliyo katika MC. Hatuelewi kama kifungu hiki kilisahaulika au yalikuwa makosa ya upigaji chapa ama mtafsiri alikosa kukitafsiri kwa sababu gani.

4.4 Matatizo ya Kisemantiki

Katika kutafsiri sheria, lazima maana ya kisheria ihifadhiwe. Maana iliyomo katika msemo wa Kiingereza ni lazima ihifadhiwe na iwepo kwa ukamilifu katika Kiswahili. Wakati mwingine ni rahisi kufahamu kifungu cha maneno kina maana gani lakini si rahisi mno kutoa maana hiyo kwa ukamilifu katika Kiswahili. Kutoa maana kamili ya kisheria ni jambo zito na mtafsiri huhitaji kuangalia maana na vijimaana vyote vilivyomo katika kifungu fulani bila ya kukipuuza hata kimoja. Ugumu wa kuchunga maana waweze kuepukika kwa kuwa mwangalifu sana. Maana ya kifungu fulani hupatikana kwa kuchunga maana za maneno yaliyotumika katika sentensi na pia maana inayojitokeza katika sentensi. Mifano tuliyotoa hapo awali kama matatizo ya kileksia na matatizo ya kisintaksia vilevile ni matatizo ya kisemantiki. Tafsiri potovu za kileksia au kisintaksia huleta upotovu

wa maana. Katika sehemu hii tutaongezea mifano mingine ya matatizo ya kisemantiki kama inavyojitokeza katika sura ya kumi na moja ya katiba.

Katika kifungu 177(1) (a), ile maana kamili ya kisheria haipo. Kwanza kifungu hiki kinahusu '*membership*' yaani uanachama. Neno hili '*membership*' limetafsiriwa Kama wanachama yaani '*members*'. Hayani maneno mawili tofauti ambayo yanaashiria vitu tofauti '*Members*' ni watu na '*membership*' ni ile hali ya kuwa mwanachama. Jambo la pili ni kuwa katika M.C wanachama hawa watachaguliwa '*on same day as a general elections of members of parliament*'. Hii ina maana kuwa watachaguliwa siku moja na ile ya uchaguzi mkuu wa wabunge. Tukiangalia tafsiri iliyotolewa, siku ile yakupiga kura ya uchaguzi mkuu wa kuchagua wabunge, kuna urudiaji mwingi unaoleta utata kwani maneno kupiga kura, uchaguzi mkuu na kuchagua wabunge yanarejelea kitu kimoja. Kisheria wabunge watachaguliwa siku ya uchaguzi mkuu na njia itakayotumika kuwachagua itakuwa ile ya kupiga kura. Jambo la tatu ni kuwa uchaguzi utafanyika '*on the second Tuesday in August in every fifth year*' yaani Jumanne ya pili ya Agosti ya kila mwaka wa tano lakini tafsiri iliyopo ni kwamba uchaguzi utafanyika baada ya miaka mitano '*after every five years*'. Kulingana na tafsiri hii basi uchaguzi utafanyika mwaka wa sita badala ya mwaka wa tano. Tafsiri hii inaleta maana isiyo kamili ya kisheria.

Matatizo mengine yanayojitokeza ni katika kifungu 188(2). Kwanza kifungu '*may be altered to take into account*' kimetafsiriwa kama inaweza kubadilishwa kwa kuzingatia lakini maana kama ilivyo katika M.C ni kuwa mipaka inaweza kubadilishwa ili kuzingatia mambo fulani yaliyoorodheshwa. Kutumia neno 'kwa' badala ya ili kunaleta tatizo la kisemantiki. Jambo la pili linalojitokeza katika kifungu hiki ni kuwa kuna mambo mawili ya kuzingatia wakati wa kubadilisha

mipaka ya kaunti kulingana na kifungu 188(b). Mambo haya ni *'physical infrastructure'* na *'human infrastructure'*. Tukiangalia tafsiri iliyotolewa, miundomsingi na uhalisia wao. Inaonekana kuwa neno lililotafsiriwa hapa ni *'infrastructure'*. Neno hili limetafsiriwa kama miundo msingi. Tafsiri hii kama ilivyo haijazingatia maneno *'physical'* na *'human'*. Tafsiri hii haionyeshi ni miundo msingi gani. Katika M.C miundo msingi hii inaeleweka wazi kama *'physical'* yaani ya kimaumbile na *'human'* ile ya kibinadamu. Kutafsiri kwa namna hii kunaleta tatizo la kisemantiki.

Tukiangalia kifungu 187(1) (b) kirai *'is not prohibited by the legislation'* kimetafsiriwa kama kunaafikiana na sheria lakini maana yake ni kuwa hakujakatazwa na sheria. Kutafsiri kifungu hiki kama kunaafikiana na sheria kunaweza kuleta utata wa maana ya kisheria. Hii ni kwa sababu kuhamisha kwa majukumu na mamlaka kunaweza kuwa kunaafikiana na sheria lakini kwa upande mwingine hakujakubaliwa au kumekatazwa.

Kunayo matatizo mawili ya kisemantiki yanayopatikana katika kifungu 180(4). Kwanza kifungu *'an election shall be held'* kimetafsiriwa kama kura zitapigwa badala ya uchaguzi utafanywa. Ingawa kwa sasa njia inayotumika kuchagua viongozi ni upigaji kura, njia hii inaweza kubadilishwa baadaye. Hapo awali njia iliyotumiwa kuwachagua viongozi ilikuwa ile ya *'mlolongo'* yaani kupiga foleni nyuma ya mgombeaji unayemtaka. Njia hii ilikuja kubadilishwa na hii ya upigaji kura iliyopo kwa sasa. Ikumbukwe kuwa katiba ni stakabadhi ambayo huchukua muda kubadilishwa na kwa hivyo hutumika kwa miaka mingi. Kuna uwezekano wa njia ya upigaji kura inayotumika kwa sasa ibadilishwe kwa njia nyingine. Kwa hivyo kutafsiri *'an election'* kama upigaji kura kunaleta utata wa kimaana.

Kwa maoni yetu ‘*an election*’ni uchaguzi unaoweza kuhusisha upigaji kura au njia yoyote nyingine. Tatizo la pili ni kutafsiri “*shall be declared elected*” kama atatangazwa kuwa mshindi. Ni kweli kuwa mtu anayechaguliwa ndiye huwa ameshinda kiti alichokuwa akiwania lakini kisheria, mgombezi hutangazwa kama aliyechaguliwa na wala sio kama aliyeshinda.

4.5 Mikakati ya Kukabiliana na Ukosefu wa Ulinganifu wa Kiistilahi

Kama tulivyokwisha kuona ukosefu wa ulinganifu wa kiistilahi ni changamoto kubwa wakati wa kutafsiri matini za kisheria kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili. Ukosefu huu huleta ukosefu wa ulinganifu wa maana. Maana ni kipengele muhimu sana kinachofaa kutiliwa maanani sana wakati wa kutafsiri matini za kisheria. Licha ya kuwa ukosefu wa ulinganifu wa kiistilahi ni changamoto kubwa hasa wakati wa kutafsiri sheria, kunayo mikakati inayoweza kutumiwa kukabiliana na changamoto hii. Mikakati hii ni kama vile kutafsiri kwa njia ya maelezo, kutohoa maneno kutoka lugha zingine, kubuni maneno mapya, kuyapa maneno ya kawaida maana za kisheria miongoni mwa njia zingine.

Katika sura ya kumi na moja ya katiba kunayo mikakati mbalimbali iliyotumiwa kukabiliana na changamoto hii. Mikakati wa kwanza uliotumiwa ni kuyachukua maneno ya Kiingereza na kuyapa miundo ya Kiswahili. Maneno haya ni kama vile;

county – kaunti

governor – gavana

senator-seneta

speaker-spika

ward-wadi.

Mkakati wa pili ni kutafsiri kwa njia ya maelezo. Kuna maneno ambayo si ya Kiingereza yaliyotumiwa katika MC. Njia mwafaka ya kutafsiri sampuli hii ya maneno ni kutoa maelezo ya maana ya maneno haya. Kwa mfano;

Ex-officio member – asiye mwanachama rasmi.

Tafsiri hii ina kasoro kwa sababu '*ex officio member*' ni mwanachama rasmi wa baraza la kaunti. Neno hili '*ex officio*' lina maana ya mwanachama aliye na mamlaka yaliyodhibitiwa. Mwanachama huyu huteuliwa kuwa spika wa baraza kwa sababu anashikilia ofisi nyingine na huwa na mamlaka yaliyodhibitiwa. Ingekuwa bora kama *ex-officio member* lingetafsiriwa kama mwanachama aliye na mamlaka yaliyodhibitiwa.

Mkakati mwingine uliotumiwa kutafsiri maneno yanayoelezea dhana hii ya ugatuzi ni uundaji wa maneno. Mfano mzuri ni neno ugatuzi ambalo ni tafsiri ya neno '*devolution*'. Dhana hii ya '*devolution*' ina maana ya kitendo cha kugawa mamlaka ya kisiasa kutoka kwa serikali kuu hadi kwa serikali za chini. Neno ugatuzi limetokana na kitenzi gatua. Kugatua ni kukata kipande kutoka sehemu kubwa. Ni kutokana na kitenzi kugatua ndipo nomino ugatuzi ikaundwa.

4.6 Hitimisho

Katika sura hii tumeangalia changamoto za kiisimu zinazotokana na ukosefu wa ulinganifu wa kiistilahi katika matini za kisheria. Tumeona kuwa ukosefu wa ulinganifu wa kiistilahi huleta upotoshi wa maana. Vilevile tumeangalia mikakati mbalimbali iliyotumika katika kukabiliana na ukosefu wa ulinganifu wa kiistilahi katika sura hii ya kumi na moja. Mikakati hii ni kama vile utohozi wa maneno,

kutafsiri kwa njia ya maelezo na uundaji wa maneno. Ni dhahiri kuwa huwezi ukapata tafsiri inayofanana kimaana moja kwa moja na matini chanzi. Kile mtafsiri hung'an'gania ni maana isipotoke sana. Mtafsiri hujaribu pawe na ulinganifu wa kimaana wa MC na ML. Ingawa kuna kasoro za tafsiri katika sura hii ya kumi na moja ya katiba tunaona kuwa mtafsiri alijaribu kutumia mikakati mbalimbali ili maana isipotoke sana.

SURA YA TANO

Hitimisho, mafanikio, matatizo na mapendekezo

5.0 Utangulizi

Katika sura hii tumetoa muhtasari wa kazi tuliyofanya katika utafiti wetu. Tumefanya hivyo kwa kuonyesha mambo mbalimbali yaliyojitokeza katika utafiti wetu. Aidha tumegusia matatizo tuliyokumbana nayo na mafanikio tuliyoyapata. Kisha tumetoa mapendekezo kuhusu utafiti zaidi.

5.1 Muhtasari

Katika tasnifu hii tumeshughulikia changamoto za kutafsiri matini za kisheria. Tumefanya hivyo kwa kutathmini sura ya kumi na moja ya Katiba ya Kenya (2010). Kazi yetu imegawanywa katika sura tano. Katika sura ya kwanza tumetanguliza somo letu la utafiti. Tumeelezea tatizo letu la utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, malengo yetu katika utafiti huu na nadharia tete. Vilevile tumeelezea msingi wa nadharia na tumedurusu yaliyoandikwa kuhusu mada yetu. Mwishowe tumefafanua njia za utafiti tulizotumia katika utafiti wetu

Katika sura ya pili tumeainisha matini za kisheria, pia tumeelezea sifa za kijumla za matini za kisheria. Vilevile tumeangalia sifa mahususi za katiba kama matini ya kisheria. Isitoshe tumeorodhesha changamoto za kutafsiri matini za kisheria kwaujumla na kuelezea mikakati inayotumiwa kukabiliana na changamoto za kutafsiri matini za kisheria. Katika sura ya tatu, tumetathmini sura ya kumi na moja ya katiba ya Kenya (2010). Tumefanya ufafanuzi wa sura hii na kuelezea dhana mbalimbali zinazohusu ugatuzi na serikali ya ugatuzi. Pia tumeorodhesha mifano ya sehemu ambazo tuliona kuwa zina tafsiri potovu.

Sura ya nne ni uchanganuzi wa data. Tumetumia mifano tuliyotoa katika sura ya tatu kuchanganua matatizo mbalimbali ya kutafsiri matini za kisheria. Tumejadili changamoto hizi katika viwango vya kiisimu vya leksia, sintaksia, semantiki na pragmatiki. Aidha tumetoa mapendekezo yetu katika baadhi ya mifano tuliyotoa. Sura ya tano ni hitimisho. Katika sura hii tumeonyesha mafanikio yetu. Vilevile tumetoa mapendekezo ya utafiti zaidi ufanywe.

5.2 Hitimisho

Kazi yetu imechunguza changamoto za kutafsiri matini za kisheria zinazoletwa na ukosefu wa ulinganifu wa kiistilahi. Tumezichunguza changamoto hizi kwa kuzichanganua kama zinavyojitokeza katika ngazi za kiisimu za leksia, sintaksia na semantiki. Tumetumia sura ya kumi na moja ya katiba ya Kenya (2010) kama kielelezo cha matini ya kisheria. Tumeitathmini sura hii na kuonyesha mifano ya matatizo haya ya kiisimu kama yanavyojitokeza. Uchunguzi wetu umedhihirisha kuwa ukosefu wa ulinganifu wa kiistilahi ni mojawapo ya changamoto mtafsiri wa kisheria hukubana nayo. Kwa vile maana hubebwa katika misingi wa kiisimu ya leksia, sintaksia na semantiki, ukosefu wa ulinganifu wa kiistilahi hujitokeza katika ngazi hizi za kiisimu na huleta upotoshi wa kimaana.

Utafiti wetu unaelekea kudhibitisha nadharia tete yetu kuwa ukosefu wa ulinganifu wa kiistilahi ni changamoto kubwa katika kutafsiri matini za kisheria. Vilevile utafiti huu umedhibitisha kuwa changamoto hizi huzua upotoshi wa maana jambo linaloweza kuleta dhuruba za kisheria. Matini ya kisheria inapotafsiriwa na maana kamili isijitokeze katika ML, wakati mwingine huhitaji wanaohusika kutafuta ufafanuzi wa kisheria mahakamani. Hii huleta gharama ya kifedha na vilevile

wakati. Kwa hivyo ni jukumu la mtafsiri wa matini za kisheria kuhakikisha kuwa tafsiri yake ina ulinganifu wa kimaana wa karibu sana na MC.

Jambo lingine ambalo tulipata kujua katika utafiti wetu ni kuwa kutafsiri sheria si jambo rahisi. Sheria ni taaluma ambayo ina istilahi zake maalum na kaida zingine za kisheria ambazo mtu wa kawaida huenda asielewe. Ili kuweza kupata ufanisi katika kutafsiri matini za kisheria, mtafsiri anafaa kuwa na ujuzi wa kimsingi katika masuala ya kisheria. Kwa hivyo watafsiri wa matini za kisheria wanafaa angalau wapate elimu ya kisheria hata kama ni ya kimsingi. Aidha walio na elimu ya kisheria nao wanaweza kushirikishwa katika shughuli za kutafsiri matini za kisheria. Wanaweza kupewa elimu ya kimsingi ya kiisimu ili waweze kuimudu kazi hii ya kutafsiri matini za kisheria.

Ingawa kutafsiri sheria hasa kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha Kiswahili kunaonekana kubanwa na matatizo mengi, uchunguzi wetu umedhihirisha kuwa, kutafsiri sheria kwa lugha wa Kiswahili ni jambo ambalo linawezekana. Tumeona kuwa Kiswahili kina maneno mengi tayari yanayoeleza dhana za kisheria. Ikiwa kuna dhana mpya ambazo hazina maneno ya Kiswahili, kuna mikakati ambayo inaweza kutumiwa ili kupata maneno ya kuelezea dhana hizi.

Uchunguzi wetu pia umeonyesha kuwa hata kama kuna matatizo ya kiisimu yanayojitokeza katika sura hii ya kumi na moja ya katiba, matatizo haya si mengi sana. Kwa hivyo tunaweza kusema kuwa, mtafsiri wa sura hii alifanikiwa kwa kiasi kikubwa katika tafsiri yake. Hakuna upotoshi mwingi wa kimaana unaojitokeza. Matatizo hayo yakirekebishwa basi, nakala hii ya katiba ya Kiswahili itaweza kutumiwa sawasawa na ile ya Kiingereza.

5.3 Mafanikio na Matatizo

Katika utafiti wetu, tulinuia kuonyesha changamoto za kutafsiri matini za kisheria zinazoletwa na ukosefu wa ulinganifu wa kiistilahi. Tulitumia tafsiri ya katiba ya Kenya (2010) hasa sura ya kumi na moja inayohusu ugatuzi. Kwa maoni yetu, tumefanikiwa kuonyesha changamoto hizi na pia kuonyesha mikakati inayoweza kutumiwa kukabiliana na ukosefu wa ulinganifu wa kiistilahi.

Katika utafiti wetu, haikuwa kazi rahisi kuchanganua changamoto zinazojitokeza katika sura ya kumi na moja ya katiba. Serikali ya ugatuzi ni dhana mpya nchini Kenya na kwa hivyo ilituhitaji kusoma kwa mapana kuhusu ugatuzi ili tuelewe vyema mfumo wa serikali ya ugatuzi na masuala yanayohusiana na ugatuzi. Tulipata tatizo la kupata vitabu na makala rejelea. Hii ni kwa sababu kazi zilizoandikwa kuhusu tafsiri za Kiswahili za kisheria ni chache mno. Tatizo lingine tulilolipata ni kutokuwa na ujuzi wa kimsingi wa kisheria. Sheria ni taaluma inayohitaji kusomewa ili mtu aweze kuelewa masuala mbalimbali ya kisheria. Hata hivyo tulijikakamua vilivyo na angalau tukapata ujuzi wa kimsingi wa kisheria hasa kuhusu usawidi wa katiba na serikali ya ugatuzi.

5.4 Mapendekezo

Upeo na mipaka yetu ilitubana katika kuchunguza changamoto za kutafsiri matini za kisheria kama zinavyojitokeza katika sura ya kumi na moja ya katiba ya Kenya 2010. Katiba ya Kenya ina sura kumi na nane. Hii ina maana kuwa kuna sura kumi na saba ambazo hatukushughulikia. Isitoshe uwanja wa sheria ni mpana mno na kwa hivyo bado kuna aina nyingi za matini za kisheria ambazo hazijashughulikiwa.

Ingesaidia sana ikiwa utafiti utafanywa wa sura hizo zingine za katiba ambazo hatukushugulikia. Vilevile ni wazi kuwa kutafsiri sheria kwa lugha ya Kiswahili ni uwanja ambao haujashughulikiwa sana na kwa hivyo utafiti mwingi unahitajika. Utafiti zaidi ukifanywa utachangia sana kupanua uelewa wa tafsiri za kisheria na vilevile tutapata makala rejelea ya kutumiwa na wasomi katika uwanja huu.

Marejeleo

Ali, S.M (1965): 'Matatizo na Matatuzi ya Kutafsiri Sheria' Swahili Vol35/1.

Dar es Salaam, University College.

Baker, M (1992). *In other words: A course book on Translation*. London,

Routledge.

Beekman, J, na Callow. J. (1974). *Translating the word of God*. Zondervan, Grand

Rapids.

Brower, R.A. (1966). *On Translation*. Cambridge, Harvard University Press

Cao, D. (2007). *Translating Law*. Amazon, Multilingual Matters.

Cartford, J.C. (1965). *A linguistic Theory on Translation*. London, O.U.P.

Gentzler.E. (2001). *Contemporary Translation Theories* (2nded).UK, Multilingual

Matters Limited.

Katiba inayopendekezwa ya Kenya, 2010, (2008), Nairobi, Government Printer.

Keenan, E. (1978). 'Some logical problems in translation' katika

Guentuner, F na G-Reutter Wan. (1978). *Meaning and Translation*

Philosophical and Linguistic Approaches. London, Duckworth.

Kelly, L. (1979). *The True Interpreter*. London, Basil Blackwell.

- Kenya Gazette Supplement No.55. (2010). *The Constitution of Kenya, 2010*. Nairobi, Government Printer.
- Larson, M.L. (1984). *Meaning-Based translation. A guide based To Cross language Equivalence*. New York, University press of America.
- Lyons, J. (1977). *Semantics*. London, Cambridge University press.
- Mlacha S.A.K. (1999). *Kamusi ya Sheria Kiingereza-Kiswahili*. Dar es saalam, Tuki.
- Newmark, P. (1988). *A Textbook of Translation*. New York, Prentice-Hall.
- Oxford Advanced Learners Dictionary*, (2008).Oxford, University Press.
- Sakareva, I. (2001, September) *Difficulties & some problems in Translating Legal Documents*, 133-138. Retrieved from <http://.w.w.w.google.com/gwtlx?wsc>.
- Snell-Hornby na Mary. S. (1986). *The Turns of Translation Studies*. Amsterdam, John Benjamin's publishing company.
- Van Dijk, B.M. (1983). *Better Translation for Better Communication*. Oxford, Pergamon Press.
- Weston A.B. (1965). 'Law in Swahili –problems developing the National language', Swahili Vol 35/2. Dar es salaam, University College.